Je! Mungu Hubadilisha Nia Yake?

. . . Mungu. Na tuendelee kusimama tukiwa tumeinamisha vichwa vyetu, kwa muda kidogo.

Baba wa Mbinguni, tunakushukuru kwa kila kitu kizuri ambacho umetupa. Hatustahili baraka Zako zo—zo zote. Hizi kweli ni baraka zisizostahiliwa ambazo tunapokea. Nasi tunaomba, Mungu, ya kwamba utaendelea kuwa pamoja nasi. Nilikuwa nimeingia tu na kuhisi roho hii nzuri sana katika mkutano huu, ninajua ianatoka Kwako. Kwa hiyo ninaomba, Baba, ya kwamba utaendelea kuutakabali mkutano huu usiku wa leo, kwa Uwepo Wako, na kuwaponya wagonjwa wote na wanaoteseka. Tujalie. Jalia huu uwe ni u—usiku mkuu ambao hatutausahau karibuni, kwa sababu ya Uwepo Wako. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

2 Ninataka kuwaomba msamaha kwa kuwachelewesha sana jana jioni. Nitajaribu kuharakisha zaidi usiku wa leo, na ili kwamba tu tuweze kuharakisha na—na kuwaombea wagonjwa. Hakika nilijisikia vizuri kuhusu mkutano wa usiku wa jana. Ilionekana kana kwamba kulikuwako na watu wengi walioponywa. Nami nilikuwa na uungwaji mkono wingi sana, kila mtu akiomba, nasi pamoja. Hivyo ndivyo tunavyosimama. Kwa hiyo, Bwana awabariki. Sasa, nafikiri, kesho usiku tutakuwa . . . Nakisia wamekwisha kutangaza hilo. Ni pengine—mahali pengine. Vema.

3 Sasa hebu na tufungue katika Kitabu cha Hesabu, mlango wa 22, upesi sana, kwa ajili ya maandiko machache tu, kutoa matamshi machache, ndipo tutatumia karibu wakati wote kwenye mstari wa maombi.

4 Billy alisema alisambaza kadi nyingi mno, kadi mia mbili ama mia tatu. Nami itanichukua muda mrefu sana kuumaliza mstari wa maombi, kwa hiyo ni—nitazungumza kwa muda mfupi, si zaidi ya dakika thelathini, ikiwezekana, halafu nitaanza mstari wa maombi, niwaombee wagonjwa. Katika Kumbukumbu la Torati, katika . . . Samahani.

5 Hesabu, mlango wa 22 na kifungu cha 31, ninataka kusoma haya.

> *Ndipo Bwana akafunua macho ya Balaamu akamwona malaika wa Bwana amesimama njiani, ana upanga mkononi mwake, umekwisha kufutwa naye akainama kichwa, akaanguka kifudifudi.*

6 Sasa hili linaweza kusikika kama andiko dogo kali kwa kuninii tu—kutoa msimamo na kuwa na ibada yetu ya uponyaji. Nami nitajaribu kuwa na mstari wa maombi uanzie ifikapo saa tatu, ikiwezekana. Sasa ninataka kuchukua somo usiku wa leo: *Je! Mungu Hubadilisha Nia Yake?*

7 Mnajua, tunaweza kubadilisha nia yetu, na kwa sababu sisi—sisi tunajifunza mambo mengine zaidi, tunajua tulikuwa tumekosea.

8 Bali mimi siamini ya kwamba Mungu anaweza kubadilisha nia Yake. Kwa sababu, kama akiibadilisha, basi bila shaka asingekuwa asiye na kikomo, na angeweza kufanya uamuzi mzuri zaidi kama angeweza kuibadilisha. Kwa hiyo Yeye . . . Imani niliyo nayo Kwake, ya kwamba—ya kwamba Yeye habadilishi nia Yake. Kwa maana kama Mungu wakati wo wote akifanya uamuzi, Yeye hana budi kudumu na uamuzi huo. Unaona? Na kila wakati shida hiyo hiyo ikitokea, hana budi kutenda vile vile alivyotenda mara ya kwanza, la sivyo alikosea mara ya kwanza. Unaona? Kwa hiyo inatupa mahali fulani pa kuwa na i—imani msingi. Sasa hatuwezi . . .

9 Naam, imani hata kidogo si kama jani tu linaloelea, kitu fulani ambacho unaweza kukipeperusha *hapa* na kukipeperusha nje huko ko kote. Ni kitu fulani ambacho kinapaswa kuwa ni cha hakika. Inapaswa kuwa imara. Na, sasa, siwezi kuweka imani yangu msingi wa nadharia fulani. Linapaswa kuwa ni jambo lilolothibitishwa kabla sijaweza kuwa na imani.

10 Ni kama tu mtu anapomchagua mke, wa kuoa. Mbona, yeye, hana budi kuwa na imani katika mwanamke huyo, akimwoa, bila shaka anachagua kujiletea shida nyingi. Unaona? Kwa hiyo hana budi kuninii, huna budi kuwa na imani, mambo fulani halisi, imani fulani ya kuwekea msingi juu yake; juu ya neno lake, juu ya vile mtu mwingine alivyosema, ama cho chote kile. Inapasa awe na kitu fulani cha kuwekea uso wake juu yake, kuwekea imani yake juu yake.

11 Kwa hiyo ninaona ya kwamba, kukutana na Mungu, kuna kitu kimoja tu ninachoweza kuwekea imani yangu juu yake na hicho ni Neno Lake.

12 Kwa sababu, tuna mawazo yanayotofautiana, kidogo karibu sisi sote. Tungeketi chini na kuanza kuzungumza hata juu ya chakula, mbona, tungetofautiana juu ya kitu cha kula; pia tumeumbwa tofauti, hamu zetu za chakula ni tofauti. Na kwa hiyo linayafanya makanisa yetu, tunaona yana mawazo tofauti juu ya mema na mabaya. Hilo linatupa sisi, kila mmoja, majaliwa ya kujichagulia.

13 Lakini, kwangu mimi, ni—ninaamini ya kwamba Neno la Mungu ni kweli. Wala si—siamini kwamba ni la kufasiriwa apendavyo mtu ye yote. Ninaamini ni vile tu linavyosema, hiyo ni Kweli. Na hivyo ndivyo ninavyolichukua, katika msingi tu wa

Hilo kuwa ni Neno la Mungu. Sasa, sina imani ya kutosha, labda, kulifanya lote litende kazi, bali hakika nisingetaka kumzuia mtu fulani ambaye ana imani ya kutosha kulifanya litende kazi.

14 Kama vile, kwa mfano, Henoko alikuwa na imani ya kutosha hata haikumbidi kufa. Yeye alienda tu kwenye matembezi ya alasiri, basi alichoka hapa duniani na akatembea kuapanda juu kwenda Mbinguni. Hakika ningependa kuwa na imani kama hiyo. Lakini ninatumaini ya kwamba tutapata imani hiyo siku moja, tunapokulia ndani Yake. Sasa ninii yetu . . .

15 Sababu ya mimi kupachagua mahali hapa, ni kwa sababu inaonekana kana kwamba hapa, kwangu mimi, ni moja ya mahali katika Biblia ambapo pangekuwa ma—mahali mkataa kwa ajili ya somo usiku wa leo, kwa maana inaonekana kana kwamba Mungu alibadilisha nia Yake, na kumwambia Balaamu jambo moja la kufanya kisha akamwambia jambo lingine la kufanya. Kwa hiyo nilifikiri, labda, kwa muda kidogo tu, tutajaribu kunyosha jambo hili kidogo tu, na tuone vile Yeye alivyomwambia hasa.

16 Kwa hiyo sasa kueleza hili kwa mhitasari. Tunajua ya kwamba Balaamu alikuwa na—na—nabii. Naye Balaki alikuwa mfalme wa Moabu, wakati huo. Nao hawakuwa ni makafiri, kule Moabu, walimtumikia Mungu yeye yule ambaye Israeli walimtumikia. Kwa sababu, Moabu, taifa hilo lilianzishwa na Mwana wa Lutu, kwa binti yake, na kwa hiyo walimtumikia Mungu yeye yule. Kama ukiangalia, dhabihu zao na kila kitu kilikuwa vile vile hasa, fahali, na kondoo dume, ikizungumza juu ya Kuja mara ya pili. Na sasa kama kanuni za msingi za Biblia ndicho tu Mungu anachohitaji, basi Moabu alikuwa ni wa kimsingi katika matoleo yake kama vile Israeli walivyokuwa. Bali tunawaona sasa, Israeli wako katika jukumu la kulifuata Neno la Mungu, kwenda katika nchi waliyokuwa wameahidiwa. Ndipo wakaja . . .

17 Hapa pangekuwapo na mfano wa mambo ya kawaida na ya kiroho, yakikutana. Na wakati ya kawaida na ya kiroho yanapokutana, sikuzote kuna mgongano, kwa maana yanapambana moja na lingine uso kwa uso. Nao Israeli hapa, wangeninii, ninataka kuwawakilisha kama Kanisa la kiroho; na Moabu kama kanisa la kawaida, kanisa lenye taratibu tu, tunaloita, kanisa la kawaida.

18 Na sisi sote tuna hakika ya kwamba kuna ka—kanisa, na kuna Bibi-arusi anayetoka kwenye kanisa hilo. Tunajua jambo hilo, ya kwamba hilo ni kweli.

19 Nao wanapambana hapa. Nasi tunaona ya kwamba walipopambana hapa, ilitokea katika jambo fulani ambalo ningetaka kuzungumza habari zake kwa muda kidogo. Mara walipogongana, na mmoja akaona vile huyo mwingine

alivyokuwa akifanya, kulikuwako na kuiga kukuu, mmoja kwa mwingine.

20 Na hapo ndipo tunapoliona leo, ya kwamba tunapata kuiga kwingi kupita kiasi. Na unapofanya jambo hilo, daima uko katika shida. Huwezi kuishi maisha ya mtu huyo mwingine. Hatuwezi kuigiza jambo fulani. Inatupasa tu kuwa jinsi tulivyo. Haikupasi (kamwe) kujaribu kufanya hivyo. Kama jamaa *huyu* akifanya jambo fulani; kwa sababu analifanya, unafikiri nawe unapaswa kulifanya, pia. Hufanyi hivyo. Wewe ni mtu binafsi, kwa Mungu. Nasi haitupasi kamwe kuigizana.

21 Na sasa, Israeli, wakiwa moja kwa moja katikati ya jukumu lao, wakitembea kwa amri, kwa agizo la Mungu, kwenda katika nchi ya ahadi, walipambana na Moabu, kundi lingine la waamini.

22 Nami natumaini hili halisikiki baya sana. Lakini maelezo madogo ninayotaka kufanya hapa ni kwamba, Moabu akiwa amekaa nchini, alikuwa zaidi ni kama shirika. Alikuwa na watu wake waheshimiwa, na watu wake maarufu wa. . .wa ufalme wake.

23 Lakini Israeli alikuwa tu ni m—mzururaji. Hawakuwa na mahali maalum walikoenda. Walihamahama tu kama Bwana alivyowaongoza. Sasa, ninaamini, pia, Balaamu, baadaye katika unabii wake, alisema, "Watu hao wasingekuwa miongoni mwa mataifa. Wangekuwa tu wametawanyika." Na hivyo ndivyo imekuwa daima. Nasi tunaona, mgongano ukatokea.

24 Ni kama vile tu Kaini na Habili, wao pia walikutana katika mgongano. Nao wakiwa ni ndugu, na wote wawili ni wa mama mmoja, Hawa. Nasi tunaona ya kwamba walitambua ya kwamba walikuwa ni wanadamu, nao walikuwa wametolewa nje ya Uzima, kutoka katika bustani ya Uzima. Na wote wawili walikuwa wakijaribu kupata njia ya kurudi Kule. Na kama uliangalia, hao wavulana wawili walikuwa ni wa kidini sana. Kaini alikuwa ni wa kidini tu kama Habili alivyokuwa. Na wote wawili walijenga madhabahu, kwa maneno mengine, kanisa. Wote wawili walitoa dhabihu. Wote wawili waliomba. Na wao—walimtumikia Mungu, wote wawili, ila mmoja wao alimtumikia vibaya.

25 Sasa, unaona, unaweza ukawa mwaminifu sana na hata hivyo uwe umekosea. Unaweza kukosea. "Iko njia ionekanayo kuwa sawa, lakini mwisho wake ni njia za mauti."

26 Sasa tu—tunaona ya kwamba hivi ndivyo ilivyokuwa kwa Kaini na Habili. Na wakati walipoona. . .Kaini alipoona ya kwamba dhabihu ya Habili ilipokelewa. Na, huenda nikasimamia hapa kusema, kwa nini Mungu aliipokea dhabihu yake? Ni kwa sababu kwamba—kwamba yeye alikuwa. . . Kwa ufunuo, alifahamu ya kwamba haikuwa ni matofaa, ama ninaamini sasa wanasema ni makomamanga ama kitu

fulani walichokula katika bustani ya Edeni, kilichosababisha dhambi. Naye alioana Adamu. . .ama, ninamaanisha, Habili aliamini ya kwamba ilikuwa (yeye) ni damu. Ambapo, ndivyo ilivyokuwa kweli. Naye Habili, kwa ufunuo, imani, alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora zaidi kuliko ya Kaini; ambayo Mungu alishuhudia kwa dhabihu hiyo, alikuwa ni mwenye haki. Unaona? Na Kanisa lote limejengwa juu ya ufunuo wa Kiungu wa Neno la Mungu. Ninii yote . . .

27 Yesu alisema hivyo. Siku moja, akishuka kutoka mlimani, Yeye aliwaambia wanafunzi Wake, "Nyinyi husema ya kwamba Mimi Mwana wa Adamu ni nani? Ama watu husema ya kwamba Mimi ni nani?"

28 "Na baadhi yao walisema, vema, Wewe ni 'Musa,' Wewe ni 'Eliya,' ama 'mmoja wa manabii.'"

Akasema, "Lakini ninyi mnasema kwamba Mimi ni nani?"

29 Na Petro akatoa lile tamshi kuu, "Wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai!"

30 Akasema, "Heri wewe, Simoni, mwana wa Yona." Na hapa ndipo penye ubishi mkubwa miongoni mwa waamini.

31 Sasa kanisa Katoliki linasema ya kwamba, "Hapo Yeye—Yeye alilijenga Kanisa Lake juu ya Petro, kwa kuwa alisema, 'Wewe ndiwe Petro,' jiwe dogo, 'juu ya jiwe hili, jiwe dogo, nitalijenga Kanisa Langu.'"

32 Vema, sasa, Waprotestanti zaidi sana wanaamini ya kwamba alilijenga juu ya Nafsi Yake Mwenyewe, juu ya Nafsi Yake, lile Jiwe la Pembeni. Lakini, unaona, Yeye alikuwa ndiye Jiwe la Pembeni la jengo hilo. Ninaami kile alichojenga Kanisa juu Yake . . .

33 Si kujifanya wa tofauti, bali, unaona, swali hilo lilikuwa, "Watu husema kwamba Mimi ni Nani?"

34 Na Petro akasema, "Wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai."

35 Yeye akasema, "Heri wewe, Simoni, mwana wa Yona, mwili na damu havikukufunulia hili. Hukulifahamu hili kwa kwenda Seminari. Unaona, hukufahamu hili hata kidogo kwa jambo la kijibunia la kibinadamu. Bali Baba Yangu, aliye Mbinguni, amekufunulia jambo hili. Unaona? Juu ya Mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda," ufunuo wa kiroho wa Yesu Kristo, Ambaye ni Neno. Ndipo ingekuwa ni Kweli ya Neno iliyofunuliwa kiroho, ndipo hasa Kanisa linapotulia.

36 Nafikiri huo ndio Habili alikuwa nao hapo mwanzo, ufunuo wa kiroho ya kwamba halikuwa ni tunda la kondeni wala kazi za mikono yetu, ama cho chote kile. Ilikuwa ni damu. Naye akamtolea Mungu dhabihu bora zaidi kuliko—kuliko Kaini aliyoitoa.

37 Tunaona kwa Ibrahimu na Lutu, jambo lile lile, katika chaguo, kwa sababu Lutu alishuka akaenda, wakati wakati ulipofika, wakati kanisa la kiroho na lile—na la kawaida yalipokutana katika mgongano, kwa sababu ya wachungaji. Iliwabidi wajitenge mmoja na mwingine. Na po pote jambo hili linapofanyika, linasababisha wivu.

38 Tunaona ya kwamba Habili, kwa sababu ya kuwa Mungu alikuwa amemtakabali, wala hakuitakabali dhabihu kubwa ya kupendeza ya Kaini, aliyokuwa ameifanyia kazi sana. Naye alikuwa ni wa kidini, na alisujudu na kuabudu, na kadhalika, alifanya kila kitu ambacho Habili alifanya, ila tu hakuwa na ufunuo kwamba ukweli ulikuwa ni upi. Kwa hiyo tunaona, ya kwamba wakati Mungu alipoukubali ufunuo wa Habili na dhabihu yake, ilimfanya Kaini kumwonea wivu Habili. Ndipo mauaji ya kwanza yakatokea.

39 Tunaona ya kwamba wivu ulitokea kati ya wachungaji wa Ibrahimu na wa Lutu, ndipo ikabidi watengane.

Tunaona ya kwamba Musa na Kora walikuwa na mgongano, pia.

Yesu na Yuda walikuwa na mapambano.

40 Na kama ilivyo sikuzote, limekuwa ni jambo lile lile, na ndivyo ilivyo leo, kanisa la kawaida na kanisa la kiroho yanapambana yanapokutana. Sasa, kanisa la kawaida linajaribu kujilinganisha na la kiroho, daima likiwa na uigaji wa kimwili. Lakini, kama ilivyokuwa kwa Esau na Yakobo, halitafanikiwa.

41 Mungu ameliita Kanisa Lake, akalipa jina, akalitenga. Na katika wakati linaoishi, Yeye atajifunua Kwake, kila wakati, kama tu alivyosema katika Warumi mlango wa 8, ya kwamba kujua tangu zamani ama kuchagua tangu zamani kwa Mungu kuweze kusimama imara. Kaini, ama ninamaanisha . . .

42 Esau na Yakobo, kabla hakuna hata mmoja wa wavulana hao aliyezaliwa, kabla hata hawajakuwa na nafasi ya kufanya chaguo, Mungu alisema, "Ninamchukia Esau na ninampenda Yakobo," kwa maana alijua yaliyokuwa ndani yao, tangu mwanzo. Nasi tunajua . . .

43 Weka hilo niani, Yeye anajua yaliyo moyoni mwako. Anajua yale unayomaanisha. Haidhuru tunasema nini, Yeye anajua unalomaanisha.

44 Na daima imesababisha shida. Nao, ninii . . . daima, wa kawaida daima wanajaribu, tangu Kaini alipomwangamiza Habili, wa kawaida daima wamejaribu kuuharibu ushawishi wa walio wa kiroho. Tunaona jambo lilo hilo leo, jambo lilo hilo leo. Inathibitisha ya kwamba linatoka kwa Shetani, kwa sababu ni wivu na uigaji wa Ukweli.

45 Kwa hiyo, kweli tunaamini ya kwamba Mungu kamwe habadilishi nia yake kuhusu yale aliyosema. Daima analidumisha kuwa kweli.

46 Lakini Yeye ana mapenzi ya kuruhusia. Sasa, hapo, ndipo shida ilipo. Tunajaribu kutenda kazi kwa mapenzi ya kuruhusia ya Mungu, naye ataliruhusu. Lakini pia kama tukichukua mapenzi Yake ya kuruhusia, ingawa si sahihi, Yeye atayafanya mapenzi Yake ya kuruhusia yatende kazi, pamoja, kuyatukuza mapenzi Yake makamilifu.

47 Hakuna jambo litakaloharibika, kwa Mungu. Sisi tunaninii. . . Yeye anajua mahali ambapo saa inagonga, usiku wa leo. Hakuna kosa lo lote. Kila pigo linapiga jinsi hasa linavyopaswa kufanya, kila kitu. Tunafikiri ni makosa, bali Yeye anajua ni sawa. Inapaswa kuwa hivi.

48 Ni kama hapo mwanzo, Mungu aliruhusu tu dhambi ije. Hakuninii, sio . . . Hayo hayakuwa ni mapenzi Yake makamilifu.

49 Lakini, unaona, Mungu, yule Roho mkuu, Baba, ndani Yake mlikuwamo na sifa, na vitu hivi mnavyoona vikionyeshwa sasa ni sifa Zake tu zikionyeshwa. Yeye aliishi peke Yake, hata hakuwa Mungu; Mungu alikuwa ni kitu cha kuabudiwa. Yeye alikuwa ni Yule Mkuu wa Milele. Na ndani Yake kulikuwako na sifa, kama za kuwa Baba, kuwa Mwokozi, kuwa Mponyaji. Na sasa, yeye angewezaje kwanza . . . Ilibidi awe Baba, kwa maana inathibitisha Yeye alikuwa ni Baba, bali anaishi peke Yake. Yeye pekee ni asiyepatikana na mauti. Na, sasa, bali sifa Zake hazina budi kuonyeshwa.

50 Sasa, kuwa Mwokozi, hapana budi kuwe na kitu fulani kilichopotea. Wala Mungu hawezi kupoteza kitu cho chote makusudi kisha akikomboe. Halitashamiri kwa utakatifu Wake na hukumu Yake kuu. Lakini alimweka mwanadamu katika hiari ya kujichagulia, akijua ya kwamba mwanadamu angeanguka. Na hivyo, basi, Yeye alifanyika mtu, Yeye Mwenyewe, kusudi apate kumkomboa mwanadamu aliyeanguka. Hiyo ndiyo sababu Yesu alikuwa Imanueli. Kama Mungu alimtuma mtu mwingine isipokuwa Yeye Mwenyewe, basi hiyo isingekuwa ni haki. Ilimbidi Mungu aje Mwenyewe na kupachukua mahali hapo. Wala Mungu asingeweza kushuka katika Roho na kupachukua mahali hapo, ilibidi afanyike mwili, katika mwili wa Mwanawe aliyeumbwa.

51 Naye alionyesha hapa, hapo mwanzo, ya kwamba mapenzi Yake makamilifu yalikuwa ni kumuumba mwanadamu kutoka katika mavumbi ya ardhi. Lakini, unaona, Yeye aliruhusu jinsia kuingizwa. Kamwe Yeye hakukusudia watoto wazaliwe kwa kujuana kimwili, bali liliruhusiwa, ambalo litatoweka hivi karibu.

52 Sasa tunaona ya kwamba Moabu alikuwa ni wa haramu, kwa—kwanza, kwa maana alikuwa ni mwana wa Lutu, kwa

binti yake. Sasa angalia, kama kanisa la kawaida, Moabu aliwaki-. . . anawakilisha ka—kanisa la kawaida, ndilo Moabu analowakilisha. Nao Israeli, kanisa la kiroho, sasa, Israeli, bibi-arusi, walikuwa ninii . . . wanawakilisha walioitwa watoke.

53 Kanisa Lenyewe, neno *kanisa* linamaanisha "walioitwa watoke, kutoka," wale ambao wametoka. "Tokeni kwake, enyi watu Wangu! Mkatengwe nao, asema Bwana, Nami nitawapokea Kwangu. Msiguse vitu vyao vichafu." Kanisa la Mungu limeitwa litoke katika ulimwengu, kutoka katika machafuko ya ulimwengu. Ninyi si wa ulimwenguni tena.

54 Kama nilivyokuwa nikijaribu kuwaambia ninyi, hivi majuzi usiku, ni wakati unapojua ya kwamba una arbuni ya ukombozi wa—wako wa Milele sasa hivi ndani yako, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, tayari umehuishwa ndani yako. Sasa umefufuka pamoja Naye, na tunaketi pamoja katika ulimwengu wa Roho, katika Kristo Yesu. Unaona, wewe si wa duniani tena. Kama ukiipenda dunia, na upendo wako ungali uko juu ya mambo ya duniani, basi kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako. Unaona? Tumetoka, tumewekwa huru na dunia. Hakuna tamaa tena.

55 Katika Waebrania, ninaamini mlango wa 10, ilisema, "Kulikuwako na kumbukumbu la daima la dhambi, kila mwaka, miili ya hao wanyama ilitolewa. Lakini katika kisa hiki, mwabudu akiisha kusafishwa hana tena dhamira ya dhambi, hana tena tamaa ya dhambi." Kitu hicho chote kimekuondokea, kwa kuwa umehuishwa katika Maisha mapya.

56 Na basi kanisa la kawaida ni kundi tu la watu katika madhehebu, ambao wamejiunga. Si tena . . . Hata siliiti tena "kanisa." Sitaki kuliita. Ninapenda kuliita kama "loji," loji ya Kimethodist, loji ya Kibaptisti, loji ya Kipentekoste.

57 Lakini Kanisa ni waliozaliwa mara ya pili walio katika Kristo Yesu, ambao ni viumbe vipya. Na kwa hiyo tungali tunaona ya kwamba, ya kwamba Mungu hutimiza Neno Lake.

58 Sasa Moabu waliona, Moabu waliangalia huko chini kondeni na kumwona Mungu akitenda kazi miongoni mwa watu hawa ambao hata hawakuwa ni taifa lenye utaratibu. Walikuwa tu wakielea kila mahali, toka mahali hadi mahali. Lakini jambo la kushangaza, ni kwamba, walikutana na mataifa haya na kuyateka. Kila kilichokuwa njiani mwao, walikiteka. Sasa, walikuta kwamba, Moabu akiwaangalia. Balaki, aliliangalia taifa la Israeli, na kusema, "Watu hawa wameufunika uso wote wa nchi." Akasema, "Nao wanayaramba mataifa, kama tu vile maksai anavyoiramba nyasi."

59 Nao walikuta kwamba, moja ya mambo muhimu sana ilikuwa ni jinsi walivyopata ufunuo huu mkuu, kulikuwako na nabii miongoni mwao. Walikuwa na nabii, sasa, mtu fulani aliyewaongoza. Haukuwa ni mfumo wa kujibunia kama

aliozoea, wa—wajumbe waliokuwa pamoja naye, na kadhalika, bali ilikuwa ni watu wake mashuhuri. Lakini walikuwa na ki—kiongozi, kiongozi aliyeitwa na Mungu.

60 Na, loo, ilikuwa ni siku ya huzini jinsi gani, wakati ulimwengu wa kanisa ulipouacha uongozi wa Kiungu wa Roho Mtakatifu, na kuchukua askofu ama cho chote kile kuchukua mahali pake. Ilikuwa ni siku yenye huzuni. Roho Mtakatifu ndiye anayepaswa kuwa kiongozi wa kanisa. Yeye ametumwa kuthibitisha Maneno ya Yesu Kristo, kulifanya kanisa liishi kama lilivyoishi mwanzoni.

61 Sasa muda mrefu uliopita, shule mashuhuri sana hapa katika—katika jiji hili, seminari fulani. Nao wana moja huko Phoenix. Na mmoja wa hao watu, ama baadhi ya wanafunzi, walikuwa, walinijia na kusema, "Tunakupenda, Ndugu Branham. Hatuna neno dhidi yako, hata kidogo, bali tungetaka kukunyosha tu."

62 Nami nikasema, "Vema, hakika ninapenda kunyoshwa." Kwa hiyo, na kwa hiyo nikasema, "Kama nimekoseakwa kweli sitaki kukosea; ninazungumza na watu wengi mno."

63 Naye akasema, "Vema, hii hapa shida yako." Kasema, "Unajaribu kuingiza, ama kufanya hai tena, dini ya kimitume. Wakati, dini ya kimitume ilikoma pamoja na mitume."

Ndipo nikasema, "Naam, bwana." Nikasema, "Vema, sasa kama . . . "

Yeye akasema, "Sasa, nisingebishana jambo hilo nawe."

64 Nikasema, "Wala mimi pia. Hutubishani. Haitupasi kufanya hivyo. Sisi ni ndugu."

Naye akasema, "Vema," akasema, "ningetaka tu kukusaidia."

Nikasema, "Hakika ninataka kupata usaidizi."

Naye akasema, "Sasa, unaona," akasema, "sasa ninii . . . hiyo ni kweli."

65 Nami nikasema, "Sasa, katika kuzungumza, hatupaswi kutumia vitabu vya kiada." Nikasema, "Mimi sitatumia vyangu," wala sikuwa na cho chote ila *Hiki*. Lakini kwa—kwa hiyo nikasema, "Sitatumia kitabu cha kiada, Biblia tu. Na, wewe, tunatumia tu Biblia."

Akasema, "Sawa."

66 Nikasema, "Sasa, tunaamini ya kwamba kanisa la kimitume lilianzia kwenye Siku ya Pentekoste. Je! unakubaliana na jambo hilo?

Akasema, "Naam, ninakubaliana nalo."

67 Nikasema, "Sasa tunatambua ya kwamba Mungu alilipa kanisa nguvu pale, kwa ajili ya miamsho hii ya kimitume."

68 Akasema, "Naam, huo ulikuwa ni mfumo wa Kanisa. Sasa kanisa tayari limewekwa katika utaratibu, na tuna wachungaji wetu wote, na madhehebu yetu makubwa na kadhalika. Hatuhitaji vitu hivyo tena, kuwavutia watu."

69 Nikasema, "Sasa Biblia inasema wapi jambo hilo?" Nikasema, "Hebu niambie mahali Biblia inaposema hayo." Unaona?

Naye akasema, "Vema, haisemi hayo hasa kwa njia hiyo."

70 Nikasema, "Vema, basi, siwezi kulipokea isipokuwa liseme hivyo kwa njia hiyo tu, unaona. Unaona?" Nikasema, "Sisi tunaninii. . . ." Nikasema, "Hivyo ndivyo inavyopaswa kuwa." Nikasema, "Je! unaamini ya kwamba Mungu angali anawaita watu?"

Akasema, "Ndiyo, Bwana."

71 Nikasema, "Sasa utaamini ya kwamba Biblia iko sahihi, kila jibu?"

"Naam."

72 Nikasema, "Sasa, yule mnenaji katika Siku ya Pentekoste, alikuwa ni Petro, ambaye alikuwa na funguo za kuingia katika ule Ufalme."

"Hiyo ni kweli."

73 Nami nikasema, "Sasa, vyo vyote vile uamuzi wake ulivyokuwa, Yesu alisema, 'Mtakalofunga duniani, nitalifunga Mbinguni; mtakalofungua duniani, nitalifungua Mbinguni.'"

Akasema, "Nitaamini hilo."

74 Nikasema, "Sasa, katika Matendo mlango wa 2 na kifungu cha 38, Petro aliwaambia watu hao waliokuwa wakishangaa. Watu hawa waliokuwa wakinena kwa lugha zisizojulikana. Nao walimwuliza wafanye nini wapate kuokolewa, naye akasema, 'Tubuni, kila mmoja wenu, na mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu; kwa maana ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wale walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu.' Sasa kama Mungu angali anaita, ahadi iyo hiyo ni kwa ajili yao."

75 Vema, akaja huku na alikuwa pamoja na moja la makundi ya Billy Graham hapa juu akiombea mkutano. Na kundi lao lilikuwa limeketi hapa California mahali fulani, majuma machache yaliyopita, katika maombi manyofu ya kilindi, wakiwa wamejiweka wakfu kwa Mungu, wakifunga, ndipo Roho Mtakatifu akalishukia kundi hilo lote nao wakaanza kunena katika lugha zingine. Naam.

76 Sasa yeye ni mfuasi wa moja la—la makanisa ya Kirafiki, Assemblies of God huko Tucson, Arizona. Alisema, "Loo, Ndugu Branham, ninapanda kwenda kule na kujisikia vizuri sana!"

Kasema, "Ninainua tu mikono yangu, na," kasema, "utukufu wa Mungu! Ninaimba tu!" Naye akasema, "Kamwe nisingeweza kufanya hivyo katika kanisa la Kibaptisti la Agano Jipya."

Nikasema, "Naona huwezi. Hiyo ndiyo sababu umetoka." Naam.

77 Kwa hiyo hivyo ndivyo mambo yalivyo, unaona, Mungu hudumisha Neno Lake. Asemayo, Yeye atayafanya. Mungu hana budi kudumisha Neno Lake.

78 Sasa tunaona hapa, ya kwamba, uigaji huu wa kimwili ambao Moabu alikuwa nao. Alimwona nabii huyu miongoni mwa Israeli, ambaye alikuwa anaweza kubariki, kulaani, kuongoza, na kadhalika, kwa hiyo anajaribu kujilinganisha, kwa njia ya siasa.

79 Sasa hilo ndilo hasa lililofanyika makanisani siku hizi. Wamejaribu kuyalinganisha na namna fulani ya mfumo. Huwezi kufanya hivyo.

80 Roho Mtakatifu hana budi kuwa hai Kanisani, daima, akiliongoza Kanisa kwa ajili ya wakati linaoishi, kuthibitisha Neno lililoahidiwa kwa ajili ya wakati huo. Mungu alinena Neno, tangu mwanzo, na kiasi fulani kwa ajili ya wakati *huu*, na kiasi fulani kwa ajili ya wakati *ule*, na kiasi fulani kwa nyakati *hizo*. Daima inatendeka jinsi hiyo tu. Na, unaona, na Roho Mtakatifu hana budi kuwa hai Kanisani, kulifanya Kanisa hili liishi siku Yake. Hilo halina budi kuwa hapa leo, kuthibitisha huduma hii ya siku za baadaye, ishara za siku za baadaye, kumwagwa kwa Roho Mtakatifu kwa siku za baadaye. Hana budi tu kuwa hapa kufanya jambo hilo, wala huwezi kulipata kwa utendaji kazi kupitia kwenye mifumo. Mungu ana mfumo. Yeye Ndiye ambaye ametupa Roho Mtakatifu.

81 Sasa, tunaona hapa ya kwamba Musa alikuwa na Mfalme, na Mfalme huyo alikuwa ni Mungu, aliyemtia mafuta. Naye Balaamu pia alikuwa chini ya mfalme, Balaki. Na zaidi sana ilikuwa ni kama mpango wa kisiasa, unaona, Balaki. Balaamu, nabii wa Mungu, alienda kwa Balaki apate habari toka kwake. Musa alimwendea Mungu apate habari toka Kwake. Hiyo hapo tofauti yake.

82 Hata hivyo, wote hao wawili walikuwa ni manabii, kwa kuwa wote wawili walikuwa wameitwa na Mungu; wote wawili walikutana na Mungu, wote wawili walinena na Mungu, na wote wawili walikuwa wamejazwa na Roho. Sasa ninafikia jambo muhimu, unaona. Sasa, wote wawili walikuwa ni watu waliojazwa na Roho Mtakatifu. Sasa, hiyo ni kweli. Biblia ilisema ya kwamba, "Mungu alikutana na Balaamu na akazungumza naye." Unaona?

83 Kwa hiyo tunaona, kila mmoja wa manabii hawa, wote wawili wakiwa ni manabii, watu wa Mungu, waliwajibika kwa

uongozi wao. Musa aliwajibika kwa Mungu. Naye Balaamu hapa aliwajibika kwa Balaki.

84 Angalia hapa, katika kufananisha ya kiroho na ya kawaida, jinsi lilivyokuwa kamilifu. Musa, aliyetumwa na Mungu, akitekeleza wajibu wake, anakutwa na kupewa changamoto na mtu mwingine wa Mungu. Ungeweza kuwazia hilo?

85 Lakini angalia ni njama ya namna gani waliyokuwa nayo pale. Lilikuwa ni taifa lililokuwa na mpangilio.

86 Na Musa alikuwa akiwaongoza wana wa Israeli, jinsi vile tu Mungu alivyowaambia mahali pa kwenda, wakiongozwa na Nguzo ya Moto, na Kiumbe cha kimbinguni kilichokuwa kikiongoza njia. Na Musa alikuwa akipokea taarifa zake kupitia kwa Lo—Logos, kwa yakini, iliyotoka kwa Mungu, ile Nguzo ya Moto; ambayo ilikuwa ni yule Malaika wa Agano, ambaye alikuwa ni Kristo, Mtiwa Mafuta. Naye alikuwa akipata ujumbe wake kupitia Pale, na kuutoa kwa wana wa Israeli, wakiwa njiani kuelekea kwenye nchi ya ahadi.

87 Lakini mtu huyu alikuwa ametulia kabisa, naye alikuwa na ufalme wake. Alikuwa na makanisa yake. Alikuwa na kila kitu pale pale kimepangiliwa katika utaratibu. Kwa hiyo akatuma mtu huyu aitwe, aje na kuwalaani watu hawa. Na angalia, ungeweza kuwazia, ya kwamba nabii, mtu mmoja wa Mungu akiziona kazi za Mungu zikiwa na mtu mwingine, na kujaribu ku—kuzipa kazi hizo za Mungu changamoto, wakati alijua, alipaswa kujua vizuri zaidi. Sasa Balaamu, kwanza wakati . . . Balaki alimtuma na kumwambia, "Njoo huku na uwalaani watu hawa." Sasa Balaki alifanya jambo lile lile, ama . . .

88 Balaamu, hasa, alifanya jambo ambalo lilikuwa ni sawa, alimsihi Mungu. Alimwomba Mungu, kwanza. Sasa, hivyo ndivyo alivyopaswa kufanya.

89 Na ndipo Mungu akampa jibu lake kamilifu, lililokuwa dhahiri sana, "Usiende pamoja naye! Usiwasumbue. Usiwalaani watu hao. Wamebarikiwa." Sasa, hilo linapaswa kuwa linatosha. Mungu anaposema jambo lo lote, Yeye hawezi kubadilisha hilo. Angalia, mapenzi Yake makamilifu yalikuwa, "Usiende! Usiwashambulie watu hao. Ni watu Wangu." Hayo yalikuwa ndiyo mapenzi Yake makamilifu.

90 Lakini Balaamu hakuwapenda watu hao, kwanza. Unaona, haya basi. Hivi tuna akina Balaamu wangapi siku hizi? Jambo lile lile, jambo lile lile! Wanajua vyema zaidi.

91 Walikuwa nao katika siku za Bwana wetu Yesu. Nikodemo alikuja na kusema, "Rabi, tunajua wewe ni mtu aliyetumwa kutoka kwa Mungu, ama ninii—ama mwalimu aliyetumwa kutoka kwa Mungu. Hakuna mtu angeweza kufanya mambo ufanyayo Mungu asipokuwa pamoja naye." Unaona, waliangalia. Huyo hapo Balaamu tena, unaona.

92 Sasa, Balaamu hakuwapenda watu hao. Angalia makao yake makuu. Baada ya kuwatuma baadhi ya watu wazuri kule, kumwambia, "Sasa kuna watu fulani wanaoshuka kuja hapa. Nami nasikia ya kwamba wewe ni nabii, wewe ni mtu mashuhuri, kwa hiyo wewe njoo hapa na uwalaani watu hawa."

93 Balaamu akasema, "Sasa, ngoja kidogo, mpaka nitakapoingia ndani na kuomba, na kukaa usiku kucha, labda Bwana atakutana nami Naye ataniambia." Vema, kesho yake asubuhi, Bwana alikutana naye akasema, "Usiende! Usiwalaani watu hao. Wamebarikiwa."

94 Vema, Balaamu alitoka akaenda na kusema, "Vema, siwezi kwenda, kwa kuwa Bwana aliniambia nisiende."

95 Sasa angalia wakati waliporudi, na wakatumia makao makuu, yeye apate kushuka kwenda kule na kuukomesha mkutano huu waliokuwa nao, unaona, vema, basi, wakakuta kwamba, makao makuu yalituma kundi bora zaidi la watu mashuhuri zaidi, labda askofu, mtu fulani mwingine, ama huenda ilikuwa ni mzee wa jimbo, mtu fulani alitumwa kule, "Mwambie ashuke aende akaukomeshe huo hata hivyo!" Unaona?

96 Angalia, kundi lake bora zaidi lenye ushawishi, zawadi bora zaidi, fedha nyingi zaidi, kasema, "Ninaweza kukupa wadhifa bora zaidi. Huenda nikakufanya, badala ya kuwa tu mtu wa kawaida, ninaweza kukupandisha cheo kidogo sasa. Nina haki ya kufanya jambo hilo, kwa sababu mimi ndiye mfalme hapa katika uamsho huu mkuu. Na ni—ninaweza kukufanyia jambo bora zaidi, kama tu tutafanya jambo hilo."

97 Angalia, ofa hiyo mpya ilimpofusha. Alipaswa kujua; yale Mungu aliyosema, Mungu atayafanya. Lakini ilimpofusha. Na kama nabii wa Mungu, hakupaswa kushawishiwa na kundi kama hilo. Alipaswa kutoka kwenye kundi hilo, kwanza.

98 Na kama ninazungumza na watu fulani wa Mungu hapa! Wakati wanapojaribu kukuambia kule kwenye makao makuu, ya kwamba, "Siku za miujiza zimepita," na haya tunayofanya hapa, na Bwana Yesu anatubariki, "na hilo ni kundi la ushupavu wa dini, kujichochea na mhemuko, hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu," toka katika kundi hilo, papo hapo. [Ndugu Branham anadata kidole chake—Mh.] Tokeni, kwa sababu ni Neno la Mungu likidhihirishwa. Wao wanasema, "Hakuna kitu kama siku za kimitume. Hakuna ubatizo wa Roho Mtakatifu. Huko kunena kwa lugha, hakuna lo lote hapo."

99 Loo, lakini, ndugu, usisikilize hayo! Kuna wengi kama Balaamu, leo, wameketi huko nyuma ofisini kwao, wakisoma Vitabu hivi vya Biblia na wanajua kwamba ni Kweli. Lakini hata hivyo kwa ajili tu ya wadhifa, hawatachukua msimamo wao. Ni kweli kabisa. Angalia, Mungu . . . Yeye alijua hakupaswa kuwa katika kundi hili, ama Balaamu alipaswa kujua

jambo hilo. Wao, wanatoka katika mapenzi ya Mungu. Hao jamaa watakuzungumzia wakutoe kabisa katika mapenzi ya Mungu. Unapoyapata mapenzi ya Mungu, usimwache mtu akuzungumzie akutoe kwake.

100 Nimewajua watu wazuri, wanaokuja mkutanoni, wanaponywa, kurudi. Nao wangesema, "Loo, vema, hamna lo lote. Umechochewa tu. Hamna cho chote." Nao watu wanaanza kutilia shaka. Nimeona watu wakija na kumpokea Kristo moyoni mwao, wanarudi; labda wananena kwa lugha, na kurudi. Nalo kanisa litasema, "Mbona, wewe—wewe ni aibu kwa Ukristo," na kadhalika. Na, loo, jamani, usininii, usifanye hivyo, unaona. Ondoka kwenye kundi hilo! Kaa mbali nalo.

101 Angalia, Balaamu alitumia kifungu cha bandia hapa, kwa ajili ya dhamira yake, unaona. Alisema, "Labda. Kaeni kesha usiku mwingine, na labda nitamwuliza Mungu, unaona. Labda huenda alibadilisha nia Yake."

102 Lakini Mungu habadilishi nia Yake. Wakati Mungu alipotupa tangazo la ubatizo wa Roho Mtakatifu, kwenye Siku ya Pentekoste, hivyo ndivyo inavyombidi kulidumisha. Alifanya hivyo kote kote katika wakati wa Biblia, Naye atafanya hivyo wakati mwingine wo wote ambapo mwanadamu atakuja katika misingi hiyo hiyo aliyoitoa pale. Kama utakuja, ukiamini, ukitubu, ukibatizwa katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zako, na ukimwamini Mungu, Mungu anawajibika kukutimizia maagizo hayo, naam, maana Yeye ni Daktari. Naye atayatimiza kama wewe—kama wewe utayatii.

103 Lakini huwezi kujaribu sasa kupata maagizo haya, uyapeleke kwa bingwatapeli wa madawa ambaye huenda—huenda akaweka kitu kingine ndani yake. Huenda kikamwua mgonjwa. Hiyo ndiyo sababu tuna wafuasi wengi sana wa kanisa waliokufa leo, wao wanajaribu kuwapa maagizo mabaya. Mungu anayo maagizo papa hapa katika Biblia. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Unapaswa kunywa dawa jinsi ambavyo Daktari alisema itolewe.

104 Biblia ilisema, "Je! hakuna—hakuna zeri katika Gileadi; je! huko hakuna tabibu?" Hakika, yuko. Kasema, "Mbona basi binti ya watu Wako yuko katika hali hii?"

105 Unaona, tuna Biblia. Tuna yule Tabibu. Ni, ninii tu, mwuza dawa anajaza vibaya maagizo ya Maandiko. Hiyo ndiyo sababu yake. Unajaribu kusema, "Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu na mambo yote haya. Ni upuuzi." Biblia iko sahihi kabisa. Mungu haghairi jambo lo lote alilosema. Nao wanajaribu kutumia njia ya bandia wakwepe, kitu kama, "Vema, tunaamini *hivyo*." Vema, haidhuru unaamini nini!

106 Ni vile Mungu alivyosema! Yeye alisema, "Nitaimwaga Roho yangu juu ya wote wenye mwili." Yeye aliahidi jambo hili katika siku za mwisho.

107 Wanajaribu kusema eti mikutano, ambayo manaona, wananiita mimi, "mpiga ramli, mpiga ramri a—a—aliyebobea, ama Be—Beelizebuli, ama ibilisi fulani." Vema, hawana budi kusema hivyo, kwa sababu wao ni wa baba yao. Hivyo ndivyo alivyosema juu ya Yesu hapo mwanzo. Wala si sisi tunaofanya jambo hili, hata hivyo, ni Yesu yeye yule, maana ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Ni Roho Wake.

108 Loo, jambo fulani ambalo lingeweza kupita, kupita na kutimi-. . .kupita agizo Lake. Watu wengi sana wanajaribu kupita hilo. "Loo, njoo ujiunge na kanisa, mambo yatakuendea sawasawa. Sisi ni kanisa la siku nyingi. Tumekuwapo hapa kwa miaka mingi. Tulianza. . . " Naam, hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, basi kanisa Katoliki la Kirumi limewashinda ninyi nyote; wao ndio wa kwanza katika madhehebu. Walikuwa wa kwanza. Lakini, kumbukeni, sio lile Kanisa la kwanza. Walikuwa ndio madhehebu ya kwanza, na mama wa kila moja lao. Ambao, kila mmoja wao ni kinyume na Mungu. Ufunuo 17 inasema jambo lile lile, unaona. Naam, tuko katika siku za mwisho. Sasa, kumbukeni, Mungu atawaruhusu, hata hivyo, unaona, sasa.

Ndipo Balaamu, yeye aliwazia, "Vema?"

109 Ndipo Mungu akamwambia, "Nenda." Kwa nini? Mungu alijua ni kitu gani kilichokuwa moyoni mwake. Mungu alijua kwamba jambo hilo kwanza lilikuwa liko moyoni mwake, kwa hiyo akamwambia, "Endelea." Ataruhusu jambo hilo. Atakuruhusu kufanya jambo hilo. Atakubariki, mara nyingi, katika kulifanya.

110 Yeye aliwabariki hata Israeli baada ya wao. . .Neema ilikuwa tayari imewapa nabii, Nguzo ya Moto, ukombozi, ishara na maajabu, ikawatoa kutoka Misri, na kila kitu, na hata hivyo wao walitaka sheria. Mungu aliwaruhusu kuwa nayo, bali Yeye aliwalaani daima.

111 Alimwacha Balaamu aendelee jinsi vile tu alivyopaswa kufanya, bali alifanya nini? Alishuka akaenda kule na, badala ya kuwalaani hao watu, alimbidi kuwabariki watu hao. Asingeweza kulaani kile ambacho Mungu alikuwa amekibariki.

112 Nami—nami niliwaambia, nilikuwa nimalizie kwenye saa tatu. Nami niliinua macho, na wakati umewadia sasa, nami nina kitabu kilichojaa mihtasari hapa.

113 Bali ninataka kusema jambo hili, katika kufunga, ya kwamba Mungu kamwe hakubadilisha nia yake. Mapenzi Yake ya moja kwa moja yalikuwa kwamba Balaamu asiende. Na Mungu anapotoa tamshi, lazima lidumu kuwa ni kweli milele.

114 Sasa, Biblia ilisema, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Sasa, hilo halimaanishi "kwa njia fulani." Hilo linamaanisha Yeye ni yeye yule jana, leo na hata milele! Yesu alisema, katika Yohana Mtakatifu 14:12, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Yeye aliahidi, katika Marko 16, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

Wanasema, "Vema, hilo lilikuwa ni kwa mitume tu."

115 Yeye alisema, "Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Ishara hizi zitafuatana na hao, ulimwenguni kote, na kwa kila kiumbe. Katika Jina langu watatoa pepo. Watasema kwa lugha. Kama wakishika nyoka, au kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Sasa, hayo ndiyo masharti yake.

116 Unaona, tunajaribu kustahilisha jambo fulani. Tunajaribu kufanya, kustahilisha kanisa kwenye yale tunayodhani ni Neno la Mungu. Hatuwezi kustahili kwa kanisa. Inabidi kustahili kwa Mungu.

117 Daima nimesema, ni wakati mkuu wa kujilinganisha. Hebu paka vipandio vyako rangi nyekundu, nawe angalia jirani yako akivipaka vyake rangi nyekundu. Hebu baadhi yenu ninyi wanawake mvae kofia ya aina fulani, kanisani, basi angalia wanawake wengine wote wakinunua hiyo.

118 Bibi Jacqueline Kennedy alikuwa na mtindo huu hapa wa kukata nywele kichwa-maji, na hebu angalieni wanawake wote. Alivaa sketi fupi kuukuu zenye rangi ya gunia, ama vitu kama hivyo, ni kashfa kwa mwanamke kutembea barabarani, akiwa amevaa hizo zimembana namna hiyo. Hebu waangalieni wanawake wote wakifanya jambo lile lile. Ni maigizo, lakini jambo hilo limo ulimwenguni. Watu wa kanisa waliliokota, na ni aibu kwamba wanafanya jambo hilo. Ni makosa kwao kufanya hivyo, na ni fedheha. Na wakati tunapoliona likinyemelea kuingia kwa Wapentekoste, ni la aibu zaidi. Hiyo ni kweli. Lakini, unaona, kanisa linavumilia jambo hilo na kuliachilia.

119 Sasa, hatujali. Sikujali kamwe kama koti langu lilifanana na suruali yangu, wala kama tai yangu ilifanana na koti langu. Ninataka ujuzi wangu ufanane na Biblia ya Mungu na matakwa Yake. Na hivyo ndivyo sisi kama wapentekoste tunavyopaswa kufanya, ni kupata tukio letu kama tu matukio yao yalivyokuwa, kwa sababu Yeye ni Yesu yeye yule, Roho Mtakatifu yeye yule, nguvu zile zile. Yeye yu hai leo, Naye anaishi miongoni mwetu.

120 Kwa namna fulani inanikumbusha juu ya siku moja mama Yake alipokuwa ameondoka Yerusalemu, kutoka katika ibada, na baba yake wa kambo, Yusufu. Nao wakasafiri kwa muda wa siku tatu, nao wakidhani tu ya kwamba Yeye alikuwa ameandamana nao, nao wakakuta kwamba hakuwapo.

121 Na, unajua, mara nyingi ninalilinganisha jambo hilo na leo. Unajua, kanisa limekuwa na safari ya hatua tatu. Luther, Wesley, pentekoste; safari ya hatua tatu. Mungu atawapa ujumbe, kuhesabiwa haki, Luther, aliushikilia; kisha ukaja utakaso kupitia kwa Wesley; halafu ubatizo wa Roho Mtakatifu, na pentekoste. Nami sijui kama wote hatukukengeuka katika hamaki fulani mahali fulani, kujenga mambo makubwa na kufanya mambo makubwa, kama Balaamu alivyotaka kufanya; mashirika makuu, ya—yale yaliyoyashinda mengine, na *hili* zaidi, wakipeana medali za dhahabu na nyota kwa ajili ya shule ya Jumapili na kwamba ni nani angeweza kuleta wafuasi wengi kabisa zaidi ya wengine wote, na kuingiza kanisani kitu cho chote kile tu.

122 Nawaambia, kuna Kanisa moja lisilo na mnafiki ndani yake, hilo ni Kanisa la Bwana Yesu Kristo, lililobatizwa kwa Roho Mtakatifu. Hushawishiwi kuingia Mle ndani. Unazaliwa Mle ndani. Unaingizwa ndani humo na Roho Mtakatifu.

123 Walikuja kutambua. Mzazi walikuja kutambua ya kwamba Yeye hakuwa miongoni mwao.

124 Sasa katika saa hii, upeo huu wa vurugu ukiwa umeanza, wakati tunapojua ya kwamba taifa hili linatetemeka. Si taifa hili tu, bali ulimwengu unatetemeka. Ni wakati wa mwisho. Hakuna kitu kingine ninachojua kitakachotukia ila Kunyakuliwa, Kuja kwa Bwana Yesu Kristo. Kila kitu kiko tayari.

125 Nasi tunaona makusanyiko haya. Loo, pata kila baraka, mkutano huu ujao, pata kila kitu kutoka kwake unachoweza kupata, ambacho ni cha Mungu. Endapo huna Roho Mtakatifu, weka tu mwako hutaondoka hapa mpaka utakapompata. Hivyo ndivyo unavyopaswa kufanya jambo hilo. Kaa hapo, maana wewe. . .hii ni, huenda ikawa ndiyo nafasi yako ya mwisho. Huenda kusiweko na mkutano mwingine kwenye Pwani hii ya Magharibi. Huenda ikawa chini ya bahari, mnamo wakati huo, kabla ya mwingine. Kwa hiyo hatujui linaloweza kutukia, kwa hiyo sisi. . .Tunatarajia hukumu za Mungu kushuka juu ya mataifa.

126 Sasa hebu niseme jambo hili. Walidhani kwamba alikuwa pamoja nao. Lakini wakakuta kwamba, katika wakati wa matatizo makuu, ya kwamba Yeye hakuwa pamoja nao. Unaona, Yeye hakuwa pamoja nao.

127 Sasa tunaona ya kwamba, ya kwamba katika wakati ambapo jambo hili kubwa limeletwa, na tunaona ya kwamba tunakosa kitu fulani katika makanisa yetu, na hicho ni nguvu za Kristo.

128 Sasa, angalieni, sitaki kukosoa. Ninawapenda, na upendo halisi, wa kweli daima husahihisha. Sasa tunamkosa Kristo kanisani mwetu. Tunamkosa Kristo miongoni mwa Wapentekoste, ndugu zetu na dada zetu. Kuna kasoro fulani. Ile mikutano ya maombi ya mtindo wa kale waliyokuwa nayo,

siku nzima na usiku kucha, hawanayo tena. Wanawake wetu walikuwa wana nywele ndefu; hawana hizo tena. Ingekuwa ni fedheha kwa wanawake kujipaka na kutumia rangi, huko nyuma katika siku za mwanzoni, na kufanya vile wanawake hawa wanavyofanya. Jambo fulani lilienda kombo. Kristo hana kasoro, unaona, bali jambo fulani lilienda kombo. Kitu fulani kiko mahali fulani. Mimbara, ilikuwa kawaida yake, haingeruhusu kitu kama hicho, bali sasa inakiruhusu. Unaona, matatizo yanaendelea, nasi tunakosa kitu fulani.

129 Tunakosa nguvu ambazo tunapaswa kuwa nazo, ambapo ile mitambo mikubwa inapaswa kuwa ikifanya kazi, na ishara kubwa na maajabu. Vema, jengo hili linapaswa kuwa limejaa nguvu za Mungu, sasa, mpaka mwenye dhambi asingeweza kukaa humu ndani; Roho Mtakatifu akihukumu kitu hicho, upesi sana namna hiyo, kama vile Anania na Safira. Nasi tunakosa kitu fulani.

130 Sasa ni kitu gani kilitukia? Walienda kumtafuta, miongoni mwa jamaa zao, wala hawakumwona miongoni mwa jamaa zao. Kwa hiyo walimkuta wapi? Moja kwa moja kule nyuma walikomwacha Yeye.

131 Nami nafikiri, wakati kanisa letu lilipofika kwenye tamasha hili kuu la kimadhehebu ambalo tulikuwa nalo, ilibidi moja kulishinda lingine, na ilibidi kuwa na makanisa makubwa zaidi, na tabaka bora zaidi ya watu, na watu waliovalia bora zaidi, na waimbaji bora zaidi, na kusimama pale na kuninii . . .

132 Ninapenda uimbaji mzuri. Ninapenda uimbaji mzuri sana wa mtindo wa kale wa kipentekoste. Bali siwezi kuvumilia upuuzi huo wa kujibandika, kamwe haunivutii; kushikilia pumzi yako mpaka unakuwa bluu usoni, kusudi tu usikiwe. Na—naamini katika kuimba kutoka moyoni mwako, katika Roho wa Mungu, kama nilivyosikia hapa ndani muda mfupi uliopita. Unaona?

133 Ninapenda kupaaza sauti kuzuri kwa mtindo wa kale, lakini nafikiri kupiga makelele kunaweza kuendelea hata tu kama muziki unaendelea ama hauendelei. Roho wa Mungu akiwa juu ya watu, hushusha baraka na nguvu za Mungu. Ninaamini mtu anaweza kutoa ushuhuda, na kuimba na kumsifu Mungu, kazini mwao, po pote walipo. Hakika.

134 Na sasa tunakosa kitu fulani. Tutampata wapi? Moja kwa moja mahali tulipomwacha, katika Neno.

Na tuombe.

135 Baba mpenzi wa Mbinguni, moja ya siku hizi usiku tutaifunga Biblia hii kwa mara ya mwisho, wimbo wa mwisho utaimbwa, mahubiri ya mwisho yatahubiriwa, mstari wa mwisho wa maombi utafanywa, mwenye dhambi wa mwisho ataingia. Na halafu nini? Ee Mungu mpendwa, hatutaki mapenzi Yako ya kuruhusia, Baba. Jalia tutembee katika mapenzi

Yako makamilifu. Hebu tuninii tu—tusichukue tu Neno moja hapa na pale, na kulifanya liafikiane na fundisho fulani la sharti ama kanuni fulani ya imani, ama jambo fulani. Hebu na tuchukue Neno jinsi lilivyo, tukiamini Injili kamili, yote ambayo Yesu alitufundisha kufanya. Hatuamini ya kwamba matendo ya mitume yalikuwa tu ni kiuzi. Tunaamini ni Neno la Mungu, ni matendo ya Roho Wako Mtakatifu katika mitume. Nasi tunaamini ya kwamba Roho Mtakatifu yeye yule, Bwana, aliyewashukia, na jinsi walivyotenda, atafanya jambo lile lile ndani yetu, wakati atakapokuja juu yetu, kama ni Roho yeye yule.

136 Kwa hiyo ninaomba, Mungu mpendwa, ya kwamba mkutano huu ambao tuko tu katika mkesha wake, utakaoanza kesho usiku. Ninaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba utakuwa ndio mkutano mkubwa sana ambao jiji hili limepata kuwa nao, kwa sababu ya Uwepo Wako. Mbariki kila mhubiri, Ee Mungu, jalia uwe wa kutetemesha sa—sana, jalia hasira ya Mungu ingurume kutoka mimbarani. Jalia wenye dhambi wawe na hofu, watetemeke. Jalia Uwepo wa Yesu Kristo uje kihalisi sana kwa watu, hivi kwamba wanaweza tu kufunga macho yao na kumwona Yeye akitembea miongoni mwao. Tujalie hilo, Bwana.

137 Sasa, usiku wa leo, kabla tu ya jambo hili halijatukia ambalo tunaliombea. . . Mungu mpendwa, baadhi ya watoto Wako ni magonjwa. Wamejeruhiwa, na—na wameumia. Nimekuja kuwaombea. Je! utatakabali ninachokuomba, usiku wa leo, Bwana, kwa ajili ya magonjwa yao? Ninatumaini, katika Wewe, hakutakuwa na mtu dhaifu katika jengo hili wakati ibada itakapokwisha.

138 Watumishi Wako pote hapa, walioketi huko nje, wakipaza sauti, wakitupa mikono yao juu, na huku nyuma hapa kwenye jukwaa, na kusema "amina" kwa Neno. Baba, sisi ni watu ambao tu kitu kimoja. Tukuja kutoka katika mambo ya duniatoka katika hali zile baridi za kidesturi, na tumezaliwa kwa Roho. Tu hai, usiku wa leo. Na wewe ulisema, kwa sababu Wewe ni hai, sisi nasi tutakuwa ni hai pia. Nasi tunatumaini, Bwana, na kuamini kwa moyo wetu wote, kulingana na Neno, ya kwamba tumewakilishwa ndani Yako Wewe.

139 Sasa yafanye Maneno Yako kuwa halisi, usiku wa leo, kuwaponya wagonjwa, ninapowaombea, na hawa wengine wanapoomba. Tujalie, Bwana, itakuwa hivyo. Nasi tutakusifu kwa ajili ya jambo hilo. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

140 Sasa. . . [Mtu fulani anaanza kunena kwa lugha nyingine. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Asante, Baba Mungu.

141 Tunajisikia ya kwamba, kama tu vile wakati mmoja katika Biblia, walipatwa na matatizo makubwa, ndipo Roho wa Bwana akashuka juu ya mtu mmoja Naye akamwambia ambapo atamshindia adui, mahali pa kwenda. Sikilizeni jambo Hilo.

Hebu jisahihishe tu. Unaona, Roho wa Uzima aliye ndani yako, hukusahihisha kwa Neno. Unaona, kama Neno linaishi ndani yako, linajiishia moja kwa moja kupitia kwenye Neno.

142 Sasa, jana usiku nilichelewa. Sasa, ninyi ni watu wazuri sana, ninaninii tu . . . Inaonekana kana kwamba, na ninapoanza kuzeheka zaidi, la—la—laiti ningaliweza tu . . . nitakuwa pamoja nanyi milele, katika Nchi nyingine.

143 Kwa hiyo sasa tutawaombea wagonjwa, na sasa sitajaribu kuleta wengi sana kwa wakati mmoja, kama nilivyofanya jana usiku. Na sasa, Billy Paul alisambaza kitita cha kadi za maombi, nafikiri ni mia moja. Je! ulisambaza mia moja, ama mia mbili? Mia mbili. Zilikuwa zipi? C.

144 Ni nani aliye na C, namba moja? Inua mkono wako, hebu tuone kama hilo ni kweli, sasa. Kadi ya maombi, angalia kadi yako ya maombi, ina namba na—na herufi juu yake. C, namba moja, inua mkono wako. Huko juu kabisa. Vema, shuka uje huku chini. Namba mbili, tatu, nne, tano. Sasa, na, wewe, mtu fulani na aje hapa na kuwashika. Sasa tunataka kila moja ya hizo kadi za maombi, bali tunataka *wapangwe* upande huu. Moja, mbili, tatu, nne, tano. Ninaona watatu wao. Na una kadi yako ya maombi, bwana? Nne. Sasa je! kuna mwingine? Tano, je! ni mtu huyo anayekuja pale? Moja, mbili, tatu, nne, tano. C, namba moja, mbili, tatu, nne, tano. Vema, sasa njoni tu kadiri mnavyoitwa, namba yako.

145 Kwa hiyo, usiku wa jana, niliwaona kule chini, watu wakisongamana. Hatutaki jambo hilo. Hili ni kanisa, mwajua, si uwanja wa mchezo. Kwa hiyo, sisi—sisi, inawapasa kuweka utaratibu.

146 Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi. Sasa wapangeni tu wanaporudi. Sasa, kadi ya maombi sita, saba, nane, tisa, kumi. Na mtu fulani atainua mkono wake watakaponinii . . . watakapokuwa wamejipanga mstari pale. Nasi tutawaombea.

147 Ni wangapi watakaoamini pamoja nami sasa ya kwamba Bwana Yesu atafanya kazi kubwa? Nitafanya yote niwezayo. Sasa sita, saba; sita, saba, nane, tisa, kumi, kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano.

148 Sasa hebu njoni tu huku, kusudi wasije wakasongamana mara moja, unajua, na karibu nayo. Hiyo ndiyo sababu mnapewa namba hizo, kuwaweka katika utaratibu, unajua. Kuwaweka ili kwamba haitakuwa . . . Basi wakati namba yako ikiitwa, vema, unakuja tu basi. Vema, na sasa tunataka kuninii . . .

149 Sasa nataka nyote, kila mtu, kuwa na kicho kweli kweli. Na tutaomba sasa kwa kama, mpaka tutakapoweza kumaliza kuwaombea watu hawa. Wala hatujui vile ambavyo huenda Bwana atafanya. Hatujui atakayofanya. Bali tunamtarajia kufanya mambo makuu.

150 Sasa, ninaamini, kumi na tano, je! nina kiasi hicho huko hadi sasa? Billy Paulo, uko wapi? Vema. Kumi na tano, kumi na sita, kumi na saba, kumi na nane, kumi na tisa, ishirini.

151 Sasa, unaona, tayari wanasongamana. Kwa hiyo sasa nitakuwa, labda, labda ndugu fulani kunininii, kama wakati hao wanapofikia mwisho wa safu, hebu na aite namba zinazofuata, mnaona, ili kwamba isitulazimu sisi sote kusimama, kusimama pale kwa muda mrefu sana wakati tunapoomba kwa—kwa ajili ya ninii—wagonjwa. Vema. Sasa tuta—tutaninii . . . Ninataka—ninawatakeni . . .

152 Ninataka kuwazungumzia wakati wakiwapanga watu hao ili wasisongamane.

153 Sasa, mtu ye yote asije mpaka namba ya—yako iitwe. Tuliita mpaka kumi na tano, ninaamini ilikuwa hivyo, ama ishirini, kitu kama hicho hapo, nitasema mpaka ishirini, na halafu acha tungojee. Na hao watakuwa wametosha hapo kwa sasa hivi, wo wote walioko hapo.

154 Na sasa kuna kadi ngapi? Inueni mikono yenu. Na ni wangapi wasio na kadi? Inueni mikono yenu.

155 Sasa, kumbukeni, haikubidi kuwa na kadi ya maombi. Tumekuwa hapa siku mbili usiku, na kila usiku Roho Mtakatifu ametoka akaenda huko kwa wasikilizaji na kuwaponya watu, bila kuwa na kadi. Hiyo ni kweli? Kadi ya maombi inakufanyia jambo moja tu, inakusaidia kuingia kwenye mstari. Hiyo ni kweli. Bali hebu na uwe na imani, ndipo uangalie Roho Mtakatifu akitoka jukwaani, papa hapa, na kwenda moja kwa moja miongoni mwa hao wasikilizaji kule. Ni wangapi wanaojua jambo hilo kwamba ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

156 Sasa, ni—ninaamini, ninaamini kwa dhati, kama kulikuwako na kanisa lingine lo lote mbali na kanisa la Kipentekoste, ya kwamba ningeninii—ningeweza kuambatana nalo na kuamini kwalo, ningekuwa pamoja nalo, kama nilifikiri ya kwamba wao wana jambo lo lote zuri zaidi. Na mnaponisikia mimi nikisema neno kuhusu madhehebu, na mambo kama hayo, siwapingi watu hao. Ni kwa sababu . . .

157 Vipi kama ungalimwona mtu unayempenda, huko nje kwenye chomboi akielea moja kwa moja kuelekea kwenye maporomoko, na unajua ya kwamba chombo hicho kitazama pamoja naye, nawe useme, "Vema, ninampenda, bali yeye—yeye ana njia zake mwenyewe"? La, nisingeweza kufanya jambo hilo. Hilo halimo ndani yangu. Ningepiga makelele, nitoke mbio na kumshika kwa nguvu, nimrushie, nimvute upesi ndani, ama cho chote kile, ili nipate kumtoa humo, unaona.

158 Na ninajua kwamba hiyo haitaelea kwenye maporomoko. Hiyo ni kweli. Inapaswa kumrudia Kristo, kweli kabisa. Haina budi kurudi kwa—kwa Mungu. Sasa mimi—mimi . . .

159 Kila mtu hapa amekuwa kwenye mkutano wangu hapo awali, ni kweli? Inueni mikono yenu kama mmekuwa kwenye mikutano hiyo. Vema. Hakuna ye yote . . .

160 Je! kuna watu wapya wo wote ambao hawajapata kuwa katika mkutano wangu hapo awali? Inueni mikono yenu. Vema, je! mnaninii . . . Kamwe sijaninii . . . Je! hii ndiyo mara ya kwanza mmekuwa katika mmoja wa mikutano yangu? Inueni mikono yenu tena. Vema, na—na—nawaambia, mimi . . .

161 Labda afadhali nibadilishe jambo hili. [Ndugu fulani anasema, "Elezea kidogo kuhusu huduma yako."—Mh.] Vema, a—afadhali nifanye hivyo.

162 Ninyi, kwenu watu ambao ndio kwanza mwingie, ni—nitaenda kuninii . . . Itanichukua tu wakati mdogo, dakika chache zaidi. Hebu nielezee, kwa maana mtaondoka zenu mkiwa na picha potofu, mnaona.

163 Ninaamini katika kila tendo la Mungu. Bali kwa kweli ninaamini ya kwamba Biblia inatuahidi, katika siku za mwisho, ya kwamba kutakuwako, kutakuja tena, Kanisa halina budi kuja katika utaratibu ule ule lililokuwa nao, ambao Yesu aliliachia wakati alipoondoka. Unaona, ni Bibi-arusi, halina budi kurudi mahali pale. Sasa, tumepitia katika kazi kubwa za Mungu, kupitia kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, kurudishwa kwa karama. Lakini katika kuufuata ukoo wa Ibrahimu . . .

164 Sasa, mimi sina elimu, na kwa hiyo inanibidi kutumia kitu kama vile ilivyokuwa Yohana Mbatizaji. Yeye hakuwa na elimu, pia. Alienda jangwani, akiwa na umri wa miaka kama tisa, wala hakupata elimu hata kidogo. Kwa hiyo mahubiri yake yalikuwa na msingi juu ya mambo ya maumbile, "Enyi uzao wa nyoka." Unaona, hicho ndicho kitu kibaya sana alichopata kuona, na kitelezi sana, naye aliwaita hao makuhani "nyoka." Alisema, "Enyi uzao wa nyoka, ni nani aliyewaonya kuitoroka ghadhabu ijayo? Msianze kusema, 'Tuna *hiki*, na sisi ni wa *hiki*.' Mungu anaweza kutoka katika mawe haya," hayo ndiyo aliyoona kwenye ukingo wa mto, "kumwinulia Ibrahimu watoto. Na, pia, shoka," hilo ndilo alilotumia nyikani, "limewekwa kwenye shina la mti. Na kila mti usiozaa tunda jema, unakatwa." Huo ndio aliochoma moto, na kutoa kuni kwake, unaona. Lakini miti mizuri . . . Ana—anahubiri jinsi hiyo tu.

165 Kwa hiyo, katika jambo hili, ninataka ku—kulisema jinsi hii. Tuko katika wakati wa mwisho, wakati wa mavuno.

166 Sasa, katika safari ya Ibrahimu, yeye alikutana na Mungu wakati wote katika hali tofauti, na kadhalika, jambo ambalo tungeweza kulichukua na kuliweka wazi. Ninii tu, sisi ni Uzao wa Ibrahimu, kama tuko katika Kristo. Na Isaka alikuwa kweli mwa—mwanawe mdogo; alikuwa ni mwanawe, kijinsia. Lakini,

kiroho, Kristo alikuwa ni Uzao wa Ibrahimu, Uzao wake wa kifalme, imani yake.

167 Sasa tunaona ya kwamba Uzao wake wa kifalme ni, unasafiri katika safari ile ile, hiyo ni kusema, Bibi-arusi wa Kristo husafiri safari ile ile Ibrahimu aliyosafiri. Na ishara ya mwisho ambayo Ibrahimu aliona, kabla ya yule mwana wa ahadi kuja, ilikuwa ni wakati Mungu alipodhihirishwa katika mwili wa mwanadamu, na Malaika wawili wakashuka.

168 Yesu alisema, katika Luka Mtakatifu, mlango wa 17 na saba na kifungu cha 30, ya kwamba, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu." Alizungumza juu ya habari za wakati wa Nuhu. Na akasema, "Kama ilvyokuwa katika siku za Sodoma," unaona, Kuja Kwake, "ndivyo itakavyokuwa katika siku Mwana wa Adamu anapofunuliwa." Sasa, Yeye hakusema kamwe "Mwana wa Mungu" akifunuliwa. "Mwana wa Adamu!"

169 Sasa, Yesu alikuja katika majina matatu. Mwana wa Adamu, ambaye ni nabii; Mwana wa Mungu, ambaye alipitia katika wakati wa Kanisa; halafu Mwana wa Daudi. Lakini kati ya Mwana wa Mungu na Mwana wa Daudi, kulingana na Neno Lake Mwenyewe, na kulingana na Malaki 4 na Maandiko mengi, Yeye anapaswa kurudi katika Kanisa Lake, katika umbo la kimwili, katika watu, katika ninii. . .katika wanadamu, kwa njia ya kuwa nabii. Unaona?

170 Hebu angalia vile Mtu huyu alivyofanya wakati aliposhuka kuja kumwona Ibrahimu. Jambo la kwanza, Yeye alimwambia Ibrahimu kuhusu jina lake kubadilishwa, kwa sababu Yeye hakumwita Abramu, Yeye alimwita Ibrahimu. Na alipofanya hivyo, mbona, tunaona ya kwamba—ya kwamba Yeye alisema, "Yu wapi mkeo, Sara?" S-a-r-a; si S-a-r-a-i.

171 "Mbona," akasema, "yuko hemani nyuma Yako."

172 Yeye alisema sasa, yeye alikuwa ana umri wa miaka tisini na Ibrahimu alikuwa na mia moja, Naye akasema, "Sasa nitakuzuru kulingana na ahadi, wakati wa maisha."

173 Naye sara akiwa ndani, alimsikia, akisikiliza kupita kwenye ukuta wa hema, naye akacheka kimoyomoyo. Ndipo yule Malaika, Mtu aliyekuwa amesimama pale, akasema, akiitambua roho yake huko nyuma, nyuma yake, na kusema, "Kwa nini Sara akacheka, akisema kuhusu mambo haya?"

174 Vema, wakamwita Sara aje, naye akakana jambo hilo. Akasema, "Bali hakika ulicheka." Alikuwa anaogopa.

175 Sasa Yesu alisema, kabla tu ya Kuja kwa Mwana wa Mungu, ama Mwana wa. . .Kuja mara ya pili, ya kwamba wakati huu tunaopitia. . .

176 Yeye alikuja kama Mwana wa Adamu, nabii, kwa sababu hilo linatimiza Maandiko. Musa alisema, "Bwana Mungu wako atawaodokeshea nabii mithili yangu." Sote tunajua huyo

alikuwa ni Yesu. Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kwa hiyo ilibidi aje kulingana na Maandiko, nabii. Yeye kamwe hakujiita Mwana wa Mungu; alijiita Mwenyewe Mwana wa Adamu.

177 Lakini sasa ndivyo alivyo, katika wakati wa Kanisa sasa, Yeye amekuwa ni Mwana wa Mungu. Katika ule Utawala wa Miaka Elfu atakuwa Mwana wa Daudi akiketi kwenye kiti cha enzi cha Daudi. Lakini katikati ya wakati huu, tunaona kwa Maandiko, Yeye atajifunua Mwenyewe tena kama Mwana wa Adamu, nabii.

178 Maana, Neno la Bwana huwaajia manabii peke yao, katu kwa wanateolojia. Ni kwa manabii. Na Bwana alisema hakutenda neno lo lote, katika Neno Lake lisilobadilika ambalo ndio kwanza tunene habari zake, mpaka kwanza anawaonyesha manabii Wake. Na katika wakati wa mwisho, hizo mihuri saba ambazo Biblia imetia muhuri, siri saba za aina saba za Kristo wote, hazina budi kufunuliwa kwanza, nazo zinaweza kuletwa tu kwa nabii. Tumekuwa tukitazamia jambo hilo, kwa miaka mingi, nasi tunaamini ya kwamba Roho Wake yuko miongoni mwetu sasa, kwa hiyo tunaona.

179 Sasa angalia wakati Yesu alipokuja, angalia yale aliyofanya kujithibitisha Mwenyewe kuwa ndiye huyo Masihi, yule Mtiwa Mafuta. Siku moja, baada ya Yeye kupokea. . .Baba alikuwa ameshuka na kukaa ndani Yake, katika umbo la hua akishuka kutoka Mbinguni, akisema, "Huyu ni Mwanangu, mpendwa Wangu, Ambaye ninapendezwa kukaa ndani Yake."

180 Hiyo ndiyo sababu alisema, "Mimi na Baba Yangu ni Mmoja. Baba Yangu anaishi ndani Yangu. Si Mimi ninayezitenda hizo kazi; ni Baba Yangu anayeishi ndani Yangu."

181 Yohana alishuhudia, akimwona huyo Roho wa Mungu, kama hua, akishuka. Sauti ikitoka Kwake, ikisema, "Huyu ni mwanangu mpendwa Ambaye ninapendezwa kukaa ndani Yake." Unaona, Naye alikaa ndani Yake.

182 Sasa angalia wakati huduma Yake ilipoanza, ilimbidi kutenda kama Mwana wa Adamu sasa. Sasa angalia vile alivyofanya. Kulitokea mtu jina lake Simoni Petro. Jina Lake lilikuwa ni Simoni wakati huo, baadaye akaitwa Petro. Andrea alikuwa akihudhuria mkutano wa Yohana; halafu basi wakati Yesu alipokuja, Naye Yohana alikuwa amekwisha mtabulisha, alimwona Yeye. Ndipo Andrea akamwomba ndugu yake, Simoni, aambatana naye mkutanoni.

183 Na alikuwa ameambiwa na baba yao, kama vile ilivyosemwa ya kwamba, "Utakuja wakati, kabla ya Masihi halisi kuja, ambapo kutakuwako na masihi wengi wa uongo watakaoinuka." Daima mambo yamekuwa hivyo. Akasema, "Lakini, enyi wanangu, kumbukeni, Masihi halisi, mtamjua kwa sababu Yeye atakuwa kulingana na Maandiko. Atakuwa ni nabii. Sasa,

hatujakuwa na nabii kwa mamia na mamia ya miaka na mamia ya miaka, tangu Malaki. Lakini kutakuwako na watu wengi watakaotoa madai, ambapo tunajua walikuwako—kulikuwako na Yesu fulani aliyeinuka na kulichukua kundi fulani, na kadhalika. Lakini Masihi huyu halisi atakuwa ni nabii." Na Waebrania wote hufundishwa kuamini yale manabii wasemayo kwamba ni kweli.

184 [Senemu tupu kwenye kanda—Mh.] Mara moja huyo mvuvi asiye na elimu, ambaye tunaambiwa hakuwa na elimu ya kutosha kuandika jina lake mwenyewe, Biblia ilisema alikuwa "asiye na elimu wala maarifa," alimtambua huyo kuwa ni Mwana wa Mungu. Alimtambua huyo kuwa Ndiye Masihi, kwa sababu huyo hapo alikuwa ni nabii. Huyo hapoYeye Yule aliyemwambia jina lake lilikuwa ni nani, na akamwambia jina la baba yake lilikuwa ni nani. Ndipo alijua huyo hapana budi alikuwa ni nabii, maana Mtu huyo hakumjua. Naye alipewa funguo za Ufalme.

185 Na tunaona kulikuwako na wengine waliosimama pale wakisikiliza hayo, na mmoja jina lake Filipo, aliyekuwa na ninii . . . alikuwa akijifunza Biblia pamoja na rafiki mmoja, jina lake Nathanaeli, wakimtamzamia Masihi. Kwa hiyo anakimbia anazunguka mlima, yapata safari ya siku moja, kisha akarudi. Naye anampata huyu Nathanaeli kule chini ya mtini, kuomba—akiomba. Ndipo akasema, "Njoo, umwone Mtu tuliyempata, Yesu wa Nazareti mwana wa Yusufu." Kwa hiyo Nathanaeli akiwa . . . ama Filipo ama . . .

186 Nathanaeli, hasa, akiwa ni mtu mzuri, akasema, "Sasa, hivi laweza neno jema kutoka Nazareti?"

Akasema, "Vema," akasema, "njoo tu uone."

187 Sasa, hilo ni shauri jema. Njoo, ujionee mwenyewe. Usikae nyumbani na kukosoa. Njoo uone. "Yachunguzeni Maandiko, ndani yake mnadhani mna Uzima wa Milele." Yesu akasema, "Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi."

188 Kwa hiyo walipokuwa wakirudi, hapana shaka, walikuwa na mazungumzo mafupi. Yeye akamwambia, akasema, "Je! unamjua yule mvuvi ambaye asingeweza kuandika ile risiti ya zile samaki ulizozinunua siku ile? Akamwambia. Unajua baba yake alikuwa kule kanisani, jina lake lilikuwa ni Yona. Unakumbuka? Kwa hiyo, Yeye—Yeye—Yeye alimwambia kwamba alikuwa ni nani."

"Loo, lazima nione jambo hilo."

189 Kwa hiyo wakati alipoenda pale, na labda alikuwa kwenye mstari wa maombi, ambapo Yesu alikuwa. Sijui. Alikuwa ameenda Mbele za Yesu. Yesu akamwangalia, na kusema, "Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!"

190 Sasa, kwanza, unasema, "Hivi Yeye alijuaje alikuwa ni Mwisraeli? Vema, kwa sababu alikuwa amevaa?" La, la.

191 Watu wote wa Mashariki huvaa hivyo vilemba. Wanavaa namna moja. Naye akasema, "Mwisraeli."

192 Kisha akasema, "Hamna hila!" Angaliweza kuwa jambazi ama cho chote kile, ndipo angefunuliwa. Alisema, "Hamna hila ndani yake!"

193 Na kwa hiyo hilo kwa namna fulani lilimwondolea majivuno, Nathanaeli, kwa hiyo akasema, "Rabi, ulipata wapi kunijua? Mbona, si—si—sielewi na jambo hili. Ulipata wapi kunijua? Sijawahi kukutana na Wewe. Nililetwa hapa tu na Filipo. Ulipata wapi kujua jambo hilo?"

194 Akasema, "Kabla hujakuwa chini ya ule mtini, wakati ulipokuwa pale ukiomba, nilikuona." Naam. Unaona?

195 Akasema, "Rabi, wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ni Mfalme wa Israeli."

196 Yesu akasema, "Kwa sababu nilikwambia jambo hili, uliamini? Basi utaona makuu kuliko haya."

197 Sasa, kulikuwako na wale waliosimama pale. Sasa hebu niwape onyo ndogo. Kulikuwako na wale waliokuwa wamesimama pale, marabi na makuhani, nao walisema, "Mtu huyu anafanya jambo hili kwa Beelizebuli."

198 Na Yesu aligeuka na kusema, "Nitawasamehe kwa ajili ya jambo hilo," kwa kuwa kafara haikuwa imetolewa bado, "bali siku moja Roho Mtakatifu atakuja na ufanye jambo lile lile," Akasema, "na kuzungumza neno moja dhidi Yake, halitasamehewa katika ulimwengu huu wala ulimwengu ujao."

Kwa mwanamke yule kisimani, wale Wasamaria.

199 Sasa, kulikuwako na jamii tatu za watu duniani. Huenda tukawa weusi, hudhurungi, manjano, cho chote tulicho, bali tunatoka katika damu moja. Na kuna mbari tatu, ambazo zilitoka kwa Hamu, Shemu, na watu wa Yafethi; na hao ni Wayahudi, Mataifa, na Wasamaria, nusu Wayahudi na Mataifa.

200 Sasa, sisi Wamataifa, Waanglo-Sakson, tulikuwa ni makafiri, tukiabudu sanamu. Hatukuwa tukimtarajia Masihi ye yote.

201 Kwa hiyo wakati Yesu alipojidhihirisha Mwenyewe kama Mwana wa Adamu...Sasa sikilizeni kwa makini, nami nitafunga. Wakati Yesu alipokuja, Yeye alikuwa na jukumu la kuwakilisha yale nabii alisema kwamba Yeye angekuwa, kwa hiyo hapo mbele ya Israeli Yeye alijiwakilisha Mwenyewe, mbele za Petro na Nathanaeli na hao pale, kama Mwana wa Adamu.

202 Sasa Yeye anataka kupitia Samaria. Na anaenda mpaka Samaria, na huko akamkuta mwanamke ameketi kisimani.

Tunajua hadithi hiyo, na wakati yeye, wakiwa wanazungumza pamoja. Huyo mwanamke alikuja kuchota maji. Yeye akasema, "Nipe maji ninywe."

203 Naye yule mwanamke akasema, "Sasa, kuna ubaguzi hapa, hatuwezi kufanya hivi. Na mimi ni mwanamke Msamaria, na Wewe ni Myahudi. Hatuna . . . "

204 Yeye akasema, "Lakini kama ungalijua ni Nani uliyekuwa ukizungumza Naye, ungeniomba Mimi maji unywe."

205 Akasema, "Vema, kisima ni kirefu, utachota na nini?"

206 Na mazungumzo yakaendelea mpaka Yeye akaipata roho yake. Na alipoipata roho Yake, akaona shida yake ilikuwa ni nini. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa ni wangapi wenu ninyi watu wageni mnaojua kwamba hiyo ni kweli? ["Amina."] Hiyo ni kweli, hiyo ilikuwa ni kweli.

Na Yeyealisema nini? "Nenda kamwite mumeo, mje naye hapa."

Akasema, "Sina mume."

207 Ndipo akasema, "Umesema vema. Kwa kuwa umekuwa na waume watano, naye unayeishi naye sasa siye mume wako." Yule mwanamke aligeuka.

208 Sasa, hakuwa kama hao makuhani, waliosema, "Yeye ana pepo. Yeye ni mpiga ramli ama kitu fulani."

209 Aligeuka, na akasema, "Bwana, naona kwamba Wewe u nabii. Sasa, hatujakuwa na mmoja kwa muda wa miaka mia nne. Kanisa halijazoea kitu kama hiki. Lakini tunaona, naona kwamba Wewe ni nabii. Sasa, ninajua ya kwamba tunamtazamia Masihi. Na Masihi ajapo, hicho ndicho kitu atakachofanya."

210 Sasa Biblia ilisema, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Kama hiyo ilikuwa ndiyo ishara iliyotiwa mafuta ya Masihi huko nyuma, kwa Msamaria na Myahudi, sasa, kamwe haikufanywa mbele ya Mataifa. Hakuna mahali po pote katika Biblia ambapo Yesu alipata kuifanya mbele ya Mataifa. Walikuwa na miaka mia nne ya kumtazamia Masihi; sisi tumekuwa na miaka elfu mbili, pamoja na matayarisho yao, pia, kumtarajia Masihi.

211 Sasa, kama huo ndio uliokuwa utambulisho Wake kabla tu ya siku zao kuisha, hauna budi kuwa ndio utambulisho wetu, kwa sababu Yeye aliahidi Mwana wa Adamu angejifunua Mwenyewe tena katika siku ambayo ulimwengu ungekuwa kama Sodoma tena. Na mtu ye yote anajua tumefikia kwenye siku hiyo. Unaona?

212 Sasa, ninaamini ya kwamba Yesu Kristo anadumisha kila Neno. Maandiko yote yana pumzi ya Mungu. Siamini tuna haki hata moja, nasi tutahukumiwa kwa hilo, kama tukiongeza neno

moja Kwake au kuondoa Neno moja Kwake. Ufunuo 22 inasema hivyo. Ninaamini ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

213 Kwa kweli ninafurahiwa na Walutheri kwa ajili ya msimamamo wao katika siku yao, Wamethodisti kwa ajili ya utakaso katika siku yao, na Wapentekoste kwa ajili ya msimamo wao katika siku yao, bali tunaishi katika siku nyingine. Tunaishi wakati kumekuwa na shina, kishada, kapi, linalofanana sana na Ngano, bali Ngano iko ndani ya kapi. Kapi ndio kwanza limesaidia tu Ngano, limezuia jua kali lisiichome. Na sasa madhehebu yanajiondoa Kwake, kusudi ipate kujianika Mbele za Mwana, ipate kuiva. Kwa hiyo tuko—tuko ndani . . . Hakutakuwako na madhehebu mengine yatakayoinuka. Huu ndio mwisho wake. Tumekuwa, daima yapata miaka mitatu, wakati ujumbe unapoanza, wao wanauundia madhehebu.

214 Huu umekuwa ukiendelea kwa karibu miaka ishirini, wala hakuna madhehebu. Haiwezekani. Tuko katika wakati wa Ngano, wakati wa mavuno. Ninaweza kusikia kombaini havesta kubwa ikija. Tunaenda Nyumbani siku moja. "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele."

215 Sasa, mimi si Yeye, bali mimi ni mtumishi Wake. Siamini ya kwamba unawawekea watu mikono na kuwapa vipawa. "Vipawa na miito havina majuto." Vimekusudiwa tangu zamani, na Mungu, kukabiliana na wakati na majira ya wakati huo. Mwanafunzi ye yote wa Biblia anajua hiyo ni kweli. Musa alizaliwa kwa wakati unaofaa. Yeremia, kwa wakati unaofaa, hao wengine wote. Yohana Mbatizaji, wakati unaofaa. Yesu alikuja katika wakati unaofaa. Nasi tuko katika wakati unaofaa. Haya ndio yanayopaswa kutendeka.

216 Sasa, ninadai ya kwamba Yeye yu hai leo, pia na Roho Wake. Baada ya nyakati za kanisa, sisi tuko katika wakati wa kanisa la Laodikia, ule mwaliko wa mwisho, na ulio mbaya sana kuliko zote, maana Yeye alitupwa nje ya kanisa. Kumbukeni, Mwana wa Adamu, naye alitupwa nje ya kanisa; si madhehebu nje ya madhehebu, bali Mtu ametupwa nje ya madhehebu. Unaona? Hakuna wakati mwingine wa kanisa uliokuwa na jambo hilo, ni Laodikia tu. Kama wewe ni wa kiroho, utafahamu.

217 Baba yetu wa Mbinguni, sasa nimeshuhudia kweli habari Zako. Sasa kama hii ni kweli, ambayo ninajua ni kweli, Bwana, ninaamini ni kweli, Wewe shuhudia ya kwamba nimesema Kweli. Katika Jina la Yesu. Amina.

218 Nitaenda kuuliza jambo fulani, hebu kidogo tu. Sikuwa nifanye mstari wa utambuzi, kwa maana nilifikiri ninyi nyote mmekuwa katika huduma yangu. Lakini kwa ajili ya watu hawa walio hapa, hebu baadhi yenu enyi watu mlio hapo mwingie kwenye kuomba, na hebu mtu fulani mstarini, ama cho chote kile. Na sasa kama Yesu Kristo atamchukua mwanadamu huyu. Halitafanikiwa bila ya ninyi. Ninyi ndio mnaofanya jambo hilo.

219 Sasa, sikilizeni, mwanamke fulani aligusa vazi Lake, siku moja, naye akageuka, akasema, "Ni nani aliyenigusa?"

220 Wote wakasema, "Mbona, unataka kusema . . . " Ama, Petro akasema, "Mbona, umati mzima unakugusa."

221 Akasema, "Lakini naona ya kwamba nimekuwa mnyonge, ama nguvu zimenitoka." *Nguvu* ni "uweza." Kisha akasema, "Naona ya kwamba nime—nimekuwa mnyonge."

222 Na kwa hiyo akaangalia kila mahali, kwa yule mwanamke, mpaka akampata, kisha akamwambia juu ya kutokwa kwake na damu. Na kwamba yeye . . . Akasema, "Imani yako imekuokoa." Vema.

223 Sasa, ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Na Agano Jipya, Kitabu cha Waebrania, kilisema ya kwamba, "Sasa hivi Yeye ndiye Kuhani Mkuu anayefanya upatanisho kwa ajili yako, anayeweza kuchukuana nawe katika mambo yako ya udhaifu."

Sasa, hapa, ndiye huyo—huyo ni mmoja wa wagonjwa hapa? Njoo.

224 Sasa, kwa ajili ya wasikilizaji. Sifanyi jambo hili kwa kusudi la kujionyesha, enyi wapendwa. Sasa acheni kuwazia jambo hilo. Kumbukeni, ninashika mawazo yenu. Ni wangapi wanaojua hilo ni kweli, na wanaliona? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

225 Huyu hapa mwanamke ambaye si—sijapata kumwona. Sijui kitu juu ya mwanamke huyu. Labda tulizaliwa umbali wa maili nyingi mmoja kwa mwingine, na kuachana kwa miaka mingi, na hapa tumesimama usiku wa leo. Hatufahamiani. Sikujui. Sasa, sina wazo. Hapa, hii hapa—hii hapa Yohana Mtakatifu 4 tena, mwa—mwanamume anakutana na mwanamke. Sasa, mimi si Yesu wala yeye si mwanamke yule. Bali hapa pana hali inayofanana nayo. Naye alisema, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya." Sasa, sijui. Inahitaji imani ya mwanamke huyu kufanya jambo hilo. Sijui lo lote juu yake. Lakini sasa kama nimesema kile ambacho ni kweli, basi Mungu anawajibika kufanya ninii . . . kusema hii ni kweli. Sasa, nikiwa sikujui, kama Mungu wa Mbinguni . . .

226 Nami nimesema Kweli. Je! unaamini ya kwamba yale niliyosema kuhusu jambo hilo ni Kweli? Mnakubali jambo hilo kuwa ni kweli? [Huyo dada anasema, "Ninaamini jambo hilo."—Mh.] Ati unaamini jambo hilo? Nisingesimama hapa mbele ya Biblia hii Takatifu na kujaribu kumdanganya mtu fulani, mtu wa umri wangu, na nikijua ya kwamba itanibidi kukutana na Mungu huko juu Hukumuni. Hatuna budi kusimama huko, siku moja. Tunajua jambo hilo.

227 Sasa kama Mungu anaweza kunifunulia, mimi, jambo fulani maishani mwako, ambalo unajua ya kwamba sijui kitu juu yake, kwa maana sikujui. Kikiwapo, ingebidi iwe ni kitu fulani maishani mwako. Nisingejua lo lote kukihusu. Ingebidi litoke

kwenye Nguvu za kimbinguni. Na ndipo ingekuwa ni juu yako, kile ulichowazia Nguvu hizo zilikuwa ni nini.

228 Na sasa kwenu ninyi wageni. Sasa ninaushika mkono wangu. Sasa, tafadhalini msitembee-tembee sasa hivi, maana, unaona, kila mmoja wenu ni roho. Ninapogeuka, unajisikia tu kama m—mvuto kutoka kila mahali fulani. Unaona, ninyi ni—ninyi ni wanadamu na mna roho. Na wewe ni roho. Kama wewe si roho, umekufa. Kwa hiyo heshimu tu, kwa muda kidogo tu.

229 Na wewe mtu hapa, ombai. Sikuwa nikitarajia jambo hili, sikuja kamwe kwa ajili ya jambo hili usiku wa leo, hata kidogo. Nilikuja tu kuwaombea wagonjwa. Bali hao ni wageni.

230 Sasa, je! unaamini jambo hilo? Kama Bwana anaweza kuniambia shida yako ni nini, ama ni nini kimekuleta hapa, jambo fulani ambalo umefanya ama unalopaswa kuwa umefanya, ama—ama jambo lingine, basi utaamini? Vema, ninajaribu kuipata roho yako, unaona. Hivyo ndivyo ninavyojaribu kufanya. Kama alivyomfanyia yule mwanamke kisimani, alizungumza naye kidogo, unaona, alikuwa akiomba maji aya kunywa. Na hivyo ndivyo ninavyojaribu kufanya, ni kushika nia yako, sio kusoma mawazo yako; lakini nikijaribu kufanya kama alivyofanya, kujua mawazo yako.

231 Uko hapa kwa ajili ya ugonjwa wa tumbo. Unaumwa na tumbo. Hiyo ni kweli. Inua mkono wako kama hiyo ni kweli. Unaamini sasa? Si hilo tu, bali una njaa ya kitu kingine. Unataka ubatizo wa Roho Mtakatifu. Punga mkono wako kama hilo ni kweli. Unaona? Niliona Nuru hiyo ikimshukia, kisha ikarudi nyuma, unaona. Nenda ukampokee Roho Mtakatifu, katika Jina la Yesu Kristo, lile jibu.

232 Unaamini sasa, ewe mgeni? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa unasema . . .

233 Sasa hapa, unaona, wakati upako huo unapoanza, ndipo Huo hapa unaenda. Unaona, mara tu mwanamke huyo aliposimama, huyo hapo mwanamke huyo, yeye sasa hivi . . . Anatambua kuna kitu Fulani kinachomzunguka.

234 Ni wangapi waliopata kuona hiyo picha ya Nguzo ya Moto, hiyo Nuru kule? Huko Washington D.C. Unaona? Sasa natamani . . . Ni kama vile katika kiwango kingine, hivyo. Ninaingalia moja kwa moja. Ile pale inaning'inia hapa karibu na yule mwanamke. Ninaiangalia moja kwa moja.

235 Sasa, mimi simhamu kabisa mwanamke huyu. Simjui. Nami nina shaka sana kama ananijua, ila tu kwa kuwa huko nje kwenye mkutano. Hivyo tu. Lakini kama Mungu anaweza kuniambia jambo fulani kukuhusu, ama jambo fulani kama tu muda kidogo uliopita, je! utaniamini mimi kwamba ni nabii Wake, mtumishi Wake? Ungeamini jambo hilo kwa moyo wako wote? Vema, na alijalie. Wewe, unakabiliwa na upasuaji, na upasuaji huo unahusu mkono wako. Hakuna alama juu yake,

bali ni ugonjwa wa neva katika mkono wako. Huo ulisababishwa na ajali, nawe unapaswa kufanyiwa upasuaji. Hebu amini, nawe haitakubidi, kufanyiwa upasuaji kama tu ukiamini kwa moyo wako wote...[Huyo dada anasema, “Ndio, bwana.”—Mh.] Naam.

236 Iweni na imani tu sasa. Msitilie shaka kamwe. Amininі tu. Sasa, hapa, hebu mwanamke huyu mwingine zaidi, sababu mwanamke huyu yuko katika hali ya taabani. Je! mnaona ule uvuli mweusi? Ni wangapi wamepata kuona picha iliyopigwa ya uvuli mweusi wa mauti? Inaning’inia juu ya mwanamke huyu sasa hivi. Mungu asipomsaidia, yeye hawezi kuishi. Ana uvimbe. [Huyo dada anasema, “Ndio!”—Mh.] Na uvimbe huo uko kwenye ubongo. [“Ndio!”] Uh-huh. Uh-huh. Uh-huh.

237 Mungu Mpenzi, kama Wewe uko karibu sana sasa, unayejua mambo yote haya, ninaomba, Mungu Mpenzi, ya kwamba utamponya dada yetu. Jalia aishi, Baba, kwa ajili ya utukufu Wako. Ninaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

238 U hali gani? Wewe ni mtu mzuri sana. Kama mama angaliishi, angekuwa karibu na umri kama wako, nadhani. Yuko Utukufuni, usiku huu. Daima angeniombea wakati nilipoenda mkutanoni. Nilimwambia Bwana...[Dada huyo anasema, “Nina umri wa miaka themanini na tano.”—Mh.] Wasemaje mama? [“Nina umri wa miaka themanini na tano.”] Umri wa miaka themanini na tano. Nakutakia heri, dada.

239 Sasa, mimi sikufahamui kabisa, nadhani. Tumeachana umri kwa miaka mingi. Nami sikujui. Sijapata kukuona. Sisi ni watu wawili tu waliokutana hapa duniani, bali wewe ni Mkristo. Wewe ni mwamini. Maana, sababu ya mimi kujua jambo hilo, ni hisia ninayopata juu ya roho yako. Wewe ni ninii, umenikaribisha, unaona. Nami ninaamini huyo ni Roho Mtakatifu, maana anafanya kazi na matendo ya Roho Mtakatifu. Unaona? Nami ninajua kwamba ni Yeye. Ninajua jambo hili tunalozungumza habari zake ni kweli. Sasa, ninajua kwamba ni kweli.

240 Sasa, sijui ungekuwa na shida gani. Lakini kama Bwana Yesu angenifunulia shida yako, je! ungeninii...ungejua kama ilikuwa ni kweli ama si kweli, ama aniambie jambo fulani ambalo umetenda, ama ulilopaswa kutenda. Je! ungeamini ilikuwa ni Bwana Yesu yeye yule, Mungu yeye yule ambaye angeweza kumwambia Filipo mahali alipokuwa, kumwambia Simoni kwamba jina lake lilikuwa ni nani? Je! unamwamini ya kwamba ni Yeye Yule?

241 Shida yako ni shida ya matumbo. [Huyo dada anasema, “Kweli kabisa.”] Hiyo ni kweli kabisa. Sivyo? [“Ndio, bwana.”—Mh.] Je! unniamini sasa mimi kuwa ni nabii Wake? Jina lako ni Bibi Bayer, Bibi Bayer, Bayer, kama asprini ya Bayer. Hiyo

ni kweli. Umeponywa. Nenda zako, Yesu Kristo amekuponya. Mungu akubariki.

242 Je! unaamini kwa moyo wako wote...Sasa kama tu ungekuwa na imani, usitie shaka!

243 Sasa, kweli wewe hauko hapa kwa ajili yako. Uko hapa kwa ajili ya mtu mwingine. Ni mwanamume, naye hayupo hapa, ndugu fulani. Ndugu huyo yuko katika hospitali ya wenda wazimu. Chukua leso hiyo uliyo nayo mkononi mwako, wakati Roho yuko juu yako, mpelekee. Iweke juu yake, usitilie shaka, atatoka kwenye hiyo hospitali na kuwa mzima. Unaamini jambo hilo? Mungu akubariki.

244 Unasema ya kwamba, "Ulisema, 'Malaika huyo, katika siku ya mwisho pale, alikuwa amegeuza mgongo Wake.' Vema, angalia."

245 Sitamwangalia mwanamke huyu. Nimegeuza mgongo wangu. Sasa, bibi, yule aliye na mgonjwa huyu, je! unaweza kunisikia, sema, "ndio." [Huyo dada anasema, "Ndio."—Mh.] Kama Bwana Yesu atanifunulia shida yako ni nini, ninapoangalia upande huu, utajua kama ni kweli ama si kweli. Hiyo ni kweli? Je! unaamini basi ni kutimiza yale Yesu aliyosema, "Itafanywa katika siku za mwisho, kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma"? Je! utaamini? Una ugonjwa wa akina mama, ugonjwa wa wanawake. Amini kwa moyo wako wote sasa, utaondoka nawe unaweza kwenda nyumbani na ukawe mzima. Mungu akubariki.

"Kama unaweza kuamini!"

246 Je! unaamini ya kwamba Mungu ataponya ugonjwa huo wa moyo? Vema, endelea tu kutembea, ukisema, "Asante, Bwana!" Amini!

247 Unaamka asubuhi, ni vigumu kwako kusogea. Yabisi kavu ni kitu kibaya, bali Yesu Kristo ndiye Mponyaji wa yabisi kavu. Je! unaamini jambo hilo? Unashuka kwenye taxi, kwa upande, ukishuka. Ninakuona ukifanya jambo hilo. Haitakubidi kufanya hivyo tena, kama utaamini. Je! unaamini kwamba nilitumwa kwa kusudi hili? [Huyo dada anasema, "Ninaamini."—Mh.] Basi, katika Jina la Yesu Kristo, na umwache. Amina.

248 Una ugonjwa wa tumbo. Je! unaamini ya kwamba Mungu atakuacha uende nyumbani, ule chakula chako cha jioni, ujisikie vizuri kuhusu jambo hilo? Nenda zako, kula chakula chako cha jioni, amini na utajisikia vizuri.

249 Una unyonge unakuja juu yako, hiyo ni kweli, kwa maana moyo wako ni mbaya. Hiyo ni kweli. Hunao tena sasa. Nenda, amini jambo hilo.

250 Vipi kama sikusema neno moja kwako, na nilikuwekea mkono tu, je! ungeniamini mimi, pia, ya kwamba utakuwa mzima? Njoo hapa.

251 Baba Mpenzi wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamponya mwanamke huyu na kumpa afya, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

252 Ni watu wangapi hapa wanaoamini, ni wangapi wenu ninyi wageni, ninyi watu wote?

253 Wazia tu, na ni vigumu kwangu kuwaona watu wakija sasa. Kumbukeni tu, ono moja lilimfanya Bwana Yesu kuwa mdhaifu. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Mwanamke mmoja alimgusa. Danieli aliona ono naye akasumbuka niani mwake, kichwani mwake, kwa siku kadha. Ni wangapi wanaojua jambo hilo [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Unaona? Vema.

254 Sasa ni wangapi wenu ninyi watu mnaoamini jambo hilo, ya kwamba huyu ni Roho Mtakatifu? Je! mnaamini jambo hilo kwa ninii wenu wote . . . Sio mimi, sasa. Roho Mtakatifu! Sasa huyu hapa mtu anayeketi hapa anayeamini jambo hilo, pia.

255 Sasa wengine, sasa baadhi yenu wengine enyi watu mlio na hizo kadi za maombi, ninataka kila mtu ambaye atakayekuwa katika mstari huu wa maombi, simama kwa miguu yako, kwa muda kidogo tu.

256 Angalia, ninataka kuwauliza swali lenye kicho. Je! mmetubu dhambi zenu zote zilizopo? Je! mnaamini? Je! mmetubu, na m—mnaamini ya kwamba mtaponywa? Mmetubia dhambi zenu zote na kusahihisha kasoro zote? Inueni mikono yenu, kama mmefanya hivyo, mbele za Mungu, mnaamini jambo hilo.

257 Na sasa huku mmeinua mikono yenu, pia, je! mnaamini inahitaji Roho Mtakatifu, na huyu ni Roho Mtakatifu ambaye anashuhudia tu Mwenyewe miongoni mwenu? Je! mnaamini jambo hilo kwa moyo wenu wote? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaamini? Basi kila mmoja wenu anaweza kuponywa.

258 Sasa je! mna imani na matumaini katika wahudumu hawa wanaoketi hapa? Je! mnawaamini hao watu, pia? Vipi kama tukiwaombea, kila mmoja, halafu tuwaache mpitie hapa na kuwawekea mikono.

259 Jambo hili linanifanya kuwa mdhaifu sana. Hilo linaendelea tu namna hiyo, lina—linanimaliza nguvu kabisa.

260 Na ni—ninaenda Afrika ya Kusini baada ya huu. Kwa kuwa, loo, jamani, mnajua jinsi mambo yalivyo huko ambako hata huwezi kuzungumza na hao watu. Na kungekuwa na ninii . . . Tunatarajia angalau watu elfu mia tatu, mkutano mmoja.

261 Kwa hiyo ninyi aminini tu! Mko hapa Marekani, mmeliona kwa kila namna.

262 Mungu mpenzi, watu hawa ni wahitaji. Wala sijui jambo lingine ambalo ungeweza kufanya, Baba, kuwathibitishia kwa Neno Lako, ya kwamba Wewe ni Mungu asiyebadilika. Ninaamini ya kwamba tumeona mambo mengi sana makuu,

Bwana, na tukala kutoka kwenye meza Yako, Chakula kitamu sana na cha ajabu cha Uzima wa Milele, mpaka tumekuwa . . . na tumekizoea sana. Ki—kimekuwa ni kitu cha kawaida. Sisi hatuninii, hatukiendei ipasavyo, Bwana, tunapoona. Hata ninajiwazia mimi mwenyewe nikisimama hapa, ninapaswa kuwa kwenye magoti yangu, nikijua ya kwamba papa hapa huyo Roho aliyemfufua katika wafu amesimama papa hapa. Roho aliyekuwa ndani Yake alipokuwa akiishi hapa duniani, yuko papa hapa sasa. Nasi, maskini wenye dhambi wasiostahili, kwa neema Yake na rehema, Yeye aliyanunua maisha yetu. Na sisi hapa, leo, tukiendeleza kazi Yake, kama alivyosema ya kwamba tungeiendeleza kazi Yake. "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya." Ukiahidi mambo haya na kuyathibitisha, hapa katika ulimwengu huu! Bwana, ninakushukuru sana, kwamba ningeweza kuhesabiwa kama sehemu ya watu Wako, katika siku hii ya mwisho.

263 Mungu Mpenzi, watu hawa wanasimama. Wao ni wagonjwa, Baba. Sina njia ya kuwaponya. Na wala Wewe huna sasa, umewaponya tayari. Ulijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa mapigo yako sisi tuliponywa. Kwa hiyo, Baba, ninaomba ya kwamba kila mmoja wao anayepitia hapa, tutakapowaombea, ya kwamba watakuja kana kwamba walikuwa sasa wakitembea chini ya msalaba. Kwa kuwa wanajua, bila shaka yo yote, Roho Mtakatifu aliyethibitishwa yuko hapa jukwaani. Kristo wa Mungu yuko papa hapa mkutanoni. Samehe kila dhambi. Ondoa kila kutokuamini. Na jalia kila mmoja wao aponywe wanapopitia kwenye mstari huu. Katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba. Amina.

264 [Ndugu fulani anasema, "Ndugu Branham, afadhali kila mtu aketi, na tuchukue sehemu moja kwa wakati mmoja, wasije wakasongamana."—Mh.] Naam. Vema.

265 Sasa ninataka kuwauliza jambo fulani. Je! ninyi, ndugu zangu, mnaweza kusimama hapa pamoja nami?

266 Mnaona, hili hapa jambo moja juu yake. Wainjilisti wengi wanaingia mjini, nao wanafanya maombi wawezayo kwa ajili ya wagonjwa, na hayo mengine yote. Na wakati kusanyiko, wanapoondoka, ha—ha—hao watu wamejengwa tu kwa mwinjilisti huyo, unaona. Sivyo ilivyo, enyi watu. Watu hawa, natilia shaka mtu ye yote katika kizazi hiki . . . Ninajua jambo hilo, kuna uigaji mwingi sana, bali sitasema nililokuwa nikitaka kwenda kusema. Lakini huenda watu hawa wasifanye jambo hilo, hiyo ni kweli, nami ninalitilia shaka sana jambo hilo.

267 Lakini wao wamechaguliwa na Mungu vivyo hivyo, kuwawekea mikono wagonjwa, kama mimi nilivyo ama mtu mwingine ye yote. Mungu anaweza jinsi iyo hiyo kuyajibu mombi yao, kadiri anavyoweza kuyajibu maombi yo yote yaliyopo. Yesu ameagiza, "Ishara hizi," hakusema zitamfuata

William Branham, Oral Roberts, kadhalika, “zitawafuata hao waaminio.” Na watu hawa wamejazwa na Roho wa Mungu. Ni watu waliobatizwa, kwa Roho Mtakatifu yeye yule. Roho huyo aliyekuwa hapa akifanya kazi hiyo muda mfupi tu uliopita, Yeye angali yupo hapa. Yuko juu ya kila mmoja wa watu hawa, unaona, nao wote wamejazwa Naye. Kwa hiyo nitawaomba wafanye mstari maradufu hapa, kando ya safu hii hapa, wakiweza, ili kwamba waweze kuweka mikono yao juu ya wagonjwa, pia, wanapopitia hapa.

268 Nao wanataka hao walio na kadi za maombi wasimame, kadi za maombi peke yake, wasimame katika marefu ya kanisa. Na ninyi wengine mwombe, kwa dakika chache tu sasa. Simameni, kwenye kila sehemu, simameni tu moja kwa moja kwenye mkono wenu wa kushoto wa sehemu yenu. Simameni nje, kwenye sehemu yenu, ndipo watawaita tu. Mtakapouona mstari huu hapa unamalizika, hebu mstari *huu* uingie moja kwa moja ndani yake. Wakati *huu* utakapomalizika, hebu *huu* uingie badala yake.

269 Na mtakapopitia hapa sasa, kumbukeni, mtakuwa mkitembea tu isipokuwa mnaamini. Ni wangapi wenu wanajua, unajisikia tu moyoni mwako, ya kwamba umeomba vya kutosha kuhusu jambo hili, nawe utaponywa, mara utakapopitia kwenye mstari huu? Inua mkono wako, useme, “Ninakubali jambo hilo, Kristo, sasa hivi, kwa sababu tu uliagiza mambo haya.”

270 Sasa ninamwombea kila mmoja wenu. Tutaomba. Nitamwomba Dada Rose, ama ye yote yule aliye kwenye kinanda pale, Dada Rose, tafadhali utupigie, *Ni Tabibu Wa Karibu*. Na hebu watu, hao watu wengine wote, wawe katika maombi. Na wanapopitia kwenye mstari huu wa maombi, ninaamini kila mmoja ataponywa. Mungu awabariki. Ninyi wengine inamisheni vichwa vyenu, na mwe mkiwaombea wengine.

271 Iweni wanyofu kabisa. Unaona, hivyo ndivyo ambavyo maskini yule mhubiri wa Kibaptisti alivyompokea Roho Mtakatifu, hivi majuzi usiku. Alikuwa akiwazia jambo hilo, ameketi pale tu, akiwa mnyofu sana, Naye akalishukia kundi hilo lao lote. Inakupasa kuwa mwaminifu kwa Mungu.

272 Sasa Yeye amethibitisha yuko hapa pamoja nanyi. Yeye yuko hapa. ‘Sasa wakati mtu ye yote anapokwambia ya kwamba hili ni lundo tu la msisimko, unajua vyema zaidi sasa, sivyo, ninyi wageni? Yeye alijithibitisha Mwenyewe, ni Yeye. Wala hakuna mtu mwingine ye yote angaliweza kufanya jambo hilo. Jambo hili halijafanywa tangu siku za mitume. Ndio kwanza sasa lirudi kanisani, kama ilivyoahidiwa. Bwana awabariki sasa.

273 Sasa, ninyi watu, mnapopitia kwenye mstari huu, njoni, huku mkiomba. Kila mtu sasa, “Ta—tabibu mkuu amekaribia sasa, Yesu mwenye huruma.” Sasa mnapokuja, njoni huku

mmeinamisha vichwa vyenu, katika uchaji. Piteni. Watu hawa wakiwawekea mikono, mtaponywa

. . . wa juu sana katika ninii ya serafi . . .

Hiyo ni kweli. Ni sawa.

274 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . kitu. Lakini, ni jambo rahisi tu la kutii yale Mungu aliyosema ufanye. Nimeona jambo hilo likitendeka mara nyingi sana. Unaona, Maandiko hata hayakutuagiza kuwaombea watu, yalisema tu, "Wekeni mikono juu ya wagonjwa, watapata afya."

275 Hivi karibuni tu, loo, ni . . . Sisemi hivi karibuni. Kisa hicho kilikuwa mawazoni mwangu sasa. Imekuwa kama miaka mitatu ama minne iliyopita, ama zaidi. Tulikuwa papa hapa California. Wanawake wawili walipitia pale, mmoja wao alikuwa na ki—kivimbe usoni mwake, na huyo mwingine alikuwa na ugonjwa wa tumbo. Nao waliamini jambo hilo hivyo. Niliwawekea mikono, na kusema, "Sasa, ninafanya jambo hili katika Jina la Bwana Yesu."

276 Ilikuwa karibu ni mwenzi mmoja baadaye. Bibi huyo alikuwa akijaribu kula, akiwa na ugonjwa huo wa tumbo, asingeweza tu kufanya hivyo. Asubuhi moja, "hisia baridi ilipitia juu" yake, alisema, naye akaenda kula. Ndipo akakimbia kushuka kwenda kumwambia jirani yake, naye jirani yake alikuwa akitikisa mashuka, namna *hiyo*, akijaribu kutafuta kile kivimbe kilichokuwa kimeondoka usoni mwake usiku huo.

277 Unaona, aminini tu, enyi marafiki. Kama akifanya jambo hilo kwa mtu mmoja, atalifanya kwa wote. Na ni jambo rahisi tu la kuwekea mikono. Na hivyo ndivyo alivyosema tufanye. Hatujui jinsi inavyofanya kazi. Sijui jinsi linavyofanya kazi. Ni ahadi Yake tu. Alisema ingefanyika hivyo. Nami nimepata makumi elfu, kote dunia, wanapona tu. Mungu aliahidi kufanya jambo hilo, na ni ahadi Yake. Unaona, tunaamini tu jambo hilo.

278 Sasa, sote tunakuja hapa. Na ninyi ambao msingeweza kuamka, sogeeni karibu sana, nasi tunakuja kuwaombea. Sasa ninataka kila mmoja wenu ninyi wanaume mje moja kwa moja hapa, mwawekee mikono hapa, tafadhali, moja kwa moja hapa. Nami ninataka kusimama hapa na kuomba, kisha nije niwawekee mikono, pia. Vema, ingieni moja kwa moja hapa. Nyote sogeeni karibu sana, kusudi kila mtu aweze kuwafikia sasa.

279 Mungu Mpenzi, katika Jina la Yesu Kristo, tunawaombea watu hawa, baadhi yao wanateseka, wamelemaa. Pale hiyo mikono ya hao wahudumu, Bwana, inaenda mbele na nyuma kutoka kwa mmoja hadi kwa mwingine. Ninaomba ya kwamba Wewe utamponya kila mmoja wao, Bwana. Jalia Roho Mtakatifu aje juu ya hao watu, kila mmoja wao, Baba. Pia jalia Nguvu kuu za Mungu ziwafunike sasa hivi tu, na jalia waende nyumbani na wawe wazima. Tukijua jambo hili, ya kwamba Yesu

alisema, “Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Uliahidi jambo hilo, Mungu mpendwa. Tunaliamini. Tunaliamini, kwa sababu Wewe ulisema hivyo nasi tunajua kwamba ni kweli, kwa hiyo watu hawa watakuwa wazima. Katika Jina la Bwana Yesu Kristo, ninawabariki wote. Amina.

280 Mungu awabariki. [Ndugu Branham na wahudumu wanaweka mikono yao juu ya wagonjwa na kuwaombea watu. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

281 Moyo wangu unakubali uponyaji kwa ajili ya kila mmoja wenu. Ninaamini jambo hilo. Hivi mtaamini pamoja na mimi, kila mmoja wenu sasa? Hivyo tu. Niliwaambia kweli, kadiri niijuavyo. Ninawapenda, na Mungu awabariki. Nami ni—ninaamini, kwa moyo wangu wote, mtapata afya. Na baraka zangu ziwe pamoja na kila mmoja wenu sasa. Mungu na awaangalie na kuwalinda. Mko katika maombi yangu. Je! mtaniombea wakati nikiwa huko Afrika namna hiyo? Ni—ninawapenda. Nami nitawaona kesho usiku.

Je! Mungu Hubadilisha Nia Yake? SWA65-0427
(Does God Change His Mind?)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumanne jioni, tarehe 27 Aprili, 1965, kwenya mkutano wa Kimataifa wa Wafanyabiashara wa Full Gospel katika Embassy Hotel kule Los Angeles, California, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings.

SWAHILI

©2008 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org